




**Samia** ateua Mkurugenzi Mkuu mpya Usalama Taifa

UKURASA 2




UKURASA 11

# Nipashe


Jumanne Agosti 29, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581417

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




KATIBA MPYA

# Msimamo mpya serikalini washtua

• **Upinzani** wacharuka, wanasheria walonga... *Ukurasa 2*



Zitto Kabwe

Dk. Anna Henga

John Mrema

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**MAMILIONI YACHOTWA KWA KUCHEZEA MFUMO H/SHAURI**

SIKU moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa taarifa ya wizi wa mapato ya serikali kwenye halmashauri...

**UKURASA WA 3**

**MTUHUMIWA 'PANYA ROAD' AUA MJOMBA, ANYWA DAMU**

KIJANA Humphrey Shoo anayetuhumiwa kuwa mshirika wa wahalifu wa mitaani jijini Dar es Salaam 'panya road'...

**UKURASA WA 19**

KESI DADA BILIONEA MSUYA

**SHAHIDI: DCI HAKURIDHISHWA UPELELEZI, ALIONGEZA NGUVU**

MKUU wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, David Mwanahe (56), amedai mahakama kuwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa...


## STAMICO yaweka rekodi ikikusanya mapato bilioni 61/-

UKURASA 3




## Wanaotumia Flagyl kuzuia ujauzito wapewa angalizo

UKURASA 5

**MICHEZO** YANGA YATAKA MVUA YA MABAO LEO UK.24 **KATUNI** UK.6



Mwanachama wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, Tausi Msangi (kulia), akielezea wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia, jinsi kilimo kilivyowawezesha kiuchumi baada ya kukimbia vitendo vya ukatili na kuanzishiwa mradi wa kilimo cha mboga juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Msimamo mpya serikalini washtua

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI serikali ikisema inakuja na mkakati wa taifa wa elimu ya katiba kwa wananchi kwa kipindi cha miaka mitatu, wadau wamekosoa mkakati huo wakidai una lengo la kuchelewesha mchakato wa upatikanaji wake kwa sababu walizoita ni za kisiasa huku wengine wakisema muda uliowekwa kwa elimu ni mrefu.

Katika kikao cha mawaziri wa sheria na wanasheria wakuu wastaafu kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema ipo haja ikatolewa elimu kuhusu Katiba ili wananchi wasiyumbishwe na kubeba ajenda za watu wengine huku wakiacha malengo muhimu kwa ustawi wao na familia zao.

"Kwa kuwa katiba ndiyo msingi wa nchi ni lazima wananchi waijue, sasa wataijuaje, wataijua kupitia elimu, sisi kama wizara tumelipa umuhimu sana suala la elimu ili mwananchi atakapoenda kwenye mchakato wa mabadiliko tayari wajue ni nini wanabadilisha," alisema Dk. Ndumbaro.

Waziri Ndumbaro alisema ingawa wizara hiyo imekuwa ikitoa elimu, lakini kwa sasa wameamua kulipa kipaumbele suala hilo baada ya utafiti kufanyika na kuonyesha kuwa asilimia kubwa ya wananchi hawana uelewa kuhusu katiba na kubeba ajenda za wanasiasa badala ya mambo muhimu ya maendeleo yao.

"Wengine wanasema hata kuiona hawajaiona sasa ukichukulia umuhimu wa katiba katika jamii yoyote tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba hiyo asilimia zaidi ya hamsini wanaifahamu, hatari ni kwamba wasipoifahamu watachukua yale ambayo wanaambiwa yasiyo ya kweli na wakayaamini," alisema Dk. Ndumbaro.

Akizungumzia mkakati huo wa elimu ya katiba kwa wananchi, Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Itikadi na Uenezi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema, alidai ni matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kuwa wananchi walio wengi tayari wana uelewa wa kutosha kuhusu suala la katiba.

"Ni matumizi mabaya ya fedha za umma kwenda kufundisha watu wazima kuhusu katiba na pia ni kinyume na maagizo ya Rais na hata Chama Cha Mapinduzi kilichotaka mchakato uendelee leo Waziri anaturudisha darasani kwenda kujifunza kuhusu katiba, kama kweli ipo nia njema anafaa kuchukuliwa hatua ikiwamo kutenguliwa katika nafasi yake," alisema Mrema.

Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema, hauna tija kwa kuwa elimu ilikwisha kutolewa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Jaji Joseph Warioba, wakati mchakato huo ulipoanza mwaka 2011, huku akiitaka serikali kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na kikosi kazi ambacho kimekwisha kukabidhi ripoti yake kwa Rais Samia Suluhu kuhusu, masuala mbalimbali.

"Hiyo elimu ya katiba mpya wananchi walishapewa na Jaji Warioba wakati ule tena kwa miaka mitatu hiyo hiyo, tunataka serikali ipeleke bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria ya mabadiliko ya katiba, tunahitaji utekelezaji wa mapendekezo hayo kuongea sasa kumetosha," alisema.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na gazeti hili kwa simu jana alisema mpango unatia mashaka akihoji muda mrefu wa kutolewa kwa elimu hiyo na kudai una lengo la kusubiri uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 upite ndipo mchakato huo uendelee jambo ambalo alisema halina maslahi kwa wananchi.

"Ni wazo jema lakini lenye kutia mashaka hasa kutokana na urefu wa muda wa hiyo elimu..." alisema Henga.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. George Kahangwa, alidai mkakati wa elimu kwa wananchi ni ujanja wa kuchelewesha mchakato wa mabadiliko ya katiba na kusisitiza mchakato unatakiwa kuendelea kwa kupigiwa kura ya maoni baada ya kuishia katika katiba pendekezwa mwaka 2014.

"Na kama waziri anasema utafiti ndiyo umeonyesha wananchi hawana elimu ilitakiwa kwanza leo autoe huo utafiti auweke mezani, taarifa yake ya leo ingetakiwa kuhusu huo utafiti ili Watanzania waupime maana zipo pia tafiti za ujanja ujanja," alisema Dk. Kahangwa.

Wakati huo huo, ACT- Wazalendo kimeitaka serikali kuweka wazi ratiba ya utekelezaji wa maazimio ya wadau kutoka majukwaa mbalimbali, ili kuwa na Sheria Mpya ya Vyama vya Siasa, Sheria Mpya ya Uchaguzi na Marekebisho ya Sheria ya Mchakato wa Katiba mpya.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria wa chama hicho, Mbarala Maharagande, kupitia taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa Agosti 28, kutokana na majadiliano ya wadau wa siasa kupitia jukwaa la Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) cha Agosti 22 na 23, mwaka huu, alisema ni muhimu serikali ikaandaa kalenda ya utekelezaji wa maoni na maeneo yaliyofikiwa mwafaka na wadau kupitia mijadala inayohusu mageuzi yanayopaswa kufanyika katika uendeshaji wa siasa nchini.

***Imeandikwa na Enock Charles, Abeid Makarabo (UDSM) na Khadija Kategile (TUDARCo)**

# Rais samia ateua bosi mpya TISS

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemteua Balozi Ali Idi Siwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Ikulu jana, kiongozi huyo aliapishwa jana akichukua nafasi ya Said Hussein Massoro aliyeteuliwa kuwa balozi.

Januari 3 mwaka huu, Rais Samia alimteua Massoro aliyekuwa Beijing akihudumu kama Ofisa Mwandamizi wa Ubalozi wa Tanzania nchini China, akichukua wadhifa huo kutoka kwa Diwani Athumani aliyehudumu kwa miaka mitatu na miezi minne tangu serikali ya Hayati Dk. John Magufuli.

Diwani alichukua nafasi hiyo kutoka kwa Dk. Modestus Kipilimba ambaye aliteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania Namibia.

***Imendaliwa na Abeid Makarabo (UDSM) na Khadija Kategile (TUDARCo)**

# Mamilioni yachotwa kwa kuchezea mfumo halmashauri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa taarifa ya wizi wa mapato ya serikali kwenye halmashauri mbalimbali za Mkoa wa Mbeya kwa kutumia mfumo bandia wa TEHAMA, uongozi wa mkoa huo umesema imeshawakamata watu 40 wanaohusika na tuhuma hizo.

Vilevile, umesema kuwa katika ufuatiliaji wa matumizi ya mfumo huo bandia, imebaini umekuwa unatumika kwenye mikoa mitano ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Njombe na Songwe.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali Denis Mwila, alitoa taarifa hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera. Alisema mfumo huo ulibuniwa mkoani Dar es Salaam.

Alisema watuhumiwa waliokamatwa ni watumishi mbalimbali wa serikali wakiwamo madiwani, watumishi wa halmashauri, wakusanyaji mapato ya serikali na wataalamu wa TEHAMA ambao mmoja wapo ni mbunifu wa mfumo huo ambaye alikamatwa mkoani Dar es Salaam.

"Fedha zilizoibwa kupitia mfumo huu ni Sh. milioni 450 ambazo zote zimeibwa ndani ya mikoa yetu hii mitano ya Nyanda za Juu Kusini. Kwa hiyo, niwatoe hofu wananchi wa Mkoa wetu wa Mbeya kwamba mkoa wao siyo shamba la bibi kama ambavyo wengi wamekuwa wakiamini," alisema Kanali Mwila.

Alisema baadhi ya watuhumiwa ambao wamewakamata ni kutoka katika halmashauri za Mkoa wa Mbeya na wengine ni watumishi wa Halmashauri za Wilaya ya Ileje na Mamlaka ya Mji wa Tunduma mkoani Songwe.

Alisema wanaendelea kufuatilia katika maeneo hayo ili kuwakamata watu wengine ambao wamehusika katika wizi huo wa fedha za umma.

Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, Varysada Mkalimoto, alisema taasisi hiyo imeshawafikisha mahakamani watuhumiwa 20 wa wizi huo wa fedha za umma.

Alisema walianza kuwafikisha mahakamani Agosti 25 mwaka huu na walipochunguza walibaini kuwa watu hao walikuwa wameiba zaidi ya Sh. milioni 380.

Mkalimoto alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Misana Kwangula ndiye aliyebaini kuwapo mfumo huo. Alitoa taarifa kwa taasisi hiyo kwa njia ya maandishi, akiomba ufuatiliaji ufanywe.

Alisema mkurugenzi huyo alitoa taarifa Julai 12 mwaka huu baada ya kubaini mfumo huo ukitumika kwenye halmashauri yake na ndipo wakaanza kufuatilia na wakabaini kuwa ni timu ya watu wengi wamehusika.

"Katika uchunguzi, tulibaini kuwa wizi huu ulikuwa unafanyika kwa njia mbili ambazo ni mfumo wa 'bluetooth' ambao wakusanyaji ushuru walikuwa wanatumia simu zao za mkononi kuzalisha stakabadhi feki na hivyo fedha walizokuwa wanakusanya zilikuwa zikiingia mifukoni mwao," alisema Mkalimoto na kuongeza.

"Wengine walikuwa wanatumia mfumo wa tovuti, walitengeneza tovuti ambayo waliunganisha na mashine mbalimbali za kutolea risiti za kielektroniki, mmiliki wa tovuti hii ni mwananchi wa kawaida ambaye alikuwa amewaajiri wataalamu wa TEHAMA kutoka kwenye halmashauri," aliongeza.

Alisema watuhumiwa waliowafikisha mahakamani wameshtakiwa kwa makosa mbalimbali yakiwamo ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha, huku akieleza kuwa wanaendelea na taratibu za kuzishikilia mali zao kwa mujibu wa sheria.

**HABARI KITAIFA**

# STAMICO yakusanya mapato bil. 61/-

**Na Jenifer Gilla**

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk. Venance Mwasse, amesema tangu serikali kufanyia mabadiliko shirika hilo mwaka 2019 limepata mafanikio makubwa, ikiwamo makusanyo ya ndani Sh. bilioni 61.1 mwaka 2022/23 kutoka Sh. bilioni 1.3 mwaka 2018/19.

Shirika hilo limetoka kwenye hasara hadi kutengeneza faida na kuipa serikali gawio la Sh. bilioni nane jambo ambalo halijawahi kutokea tangu lianzishwe mwaka 1972.

Dk. Mwasse alisema, kutokana na mafanikio hayo shirika hilo limeondokana na utegemezi kwa kiasi kikubwa, kwa kuwa hadi kufikia mwaka 2022/23 lilikuwa linategemea serikali asilimia tisa peke kutoka asilimia 89 mwaka 2018/19 na kupata hati safi kwa miaka mitatu mfululizo kutokana na ukaguzi wa mahesabu.

Aliyasema hayo jana, wakati akielezea utekelezaji wa shughuli za shirika hilo, jijini Dar es Salaam kwa wahariri wa vyombo vya habari na kuongeza kuwa mwaka 2022/23 limetumia Sh. bilioni 17.8 kununua vifaa na mitambo ya kuchakata madini yakiwamo ya makaa ya mawe.

Alisema mafanikio hayo yametokana na mabadiliko kwenye shirika yaliyofanywa na serikali ambayo ni ya kiuongozi na kimuundo na utekelezaji wa mageuzi ya mikakati yaliyokuwa na lengo la kulifanya kuwa chombo madhubuti katika sekta ya madini yenye kulileteа taifa faida.

Pia, Dk. Mwasse alisema walifanya mapinduzi ya kiutendaji yaliyolenga kujiendesha kibiashara na kutafuta fursa za kiuwekezaji badala ya kutegemea kusaidiwa na serikali jambo lililochochea kufika hatua lilipo shirika kwa sasa.

Alisema shirika liliamsha molari za wafanyakazi, kuongeza nidhamu katika kazi na matumizi ya fedha kwa kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa pesa inayotumika kwenye uwekezaji lazima irudishe faida.

Kwa sasa shirika hilo linatekeleza miradi mbalimbali ukiwamo wa uchimbaji, uchakataji na uuzaji wa makaa ya mawe kwa wingi uliopo Kabulo Kiwira, Wilaya ya Ileje, mkoani Songwe na mradi wa kuzalisha mkaa mbadala wa kupikia kutumia makaa ya mawe ambao uzalishaji wa majaribio unaendelea jijini Dar es Salaam.

Kaimu Mkurugenzi wa Usalama na Mazingira wa shirika hilo, Rose Makame, alisema utekelezaji wa miradi hiyo unazingatia uhifadhi wa mazingira na kunufaisha wananchi wanaozunguka maeneo yenye uwekezaji huo.

"Ndio maana unaona mabaki ya makaa ya mawe tumeona tuje na teknolojia ya kutengeneza mkaa mbadala wa kupikia majumbani ili kuepusha kuyatupa na kuchafua mazingira wakati huo huo tunapunguza ukataji wa miti kiholela kwa ajili ya hitaji ya nishati ya kupikia," alisema.

Alisema mtambo wa uzalishaji mkaa mbadala ulioko TIRDO, Dar es Salaam unafanya vizuri na tayari wameshaanza kuuza sehemu mbalimbali nchini ikiwamo jijini humo na Dodoma na kuwapatia vijana na watu wenye ulemavu ajira.

Mkurugenzi wa taasisi ya Kipindi Thamani Madini, Injinia Lightness Salema, alilishauri shirika hilo kuweka mfumo wa kuuza hisa ili wananchi ambao hawajihusishi na biashara ya madini wanufaike na uwekezaji huo.

Alisema hali hiyo pia itachangia kukuza uwekezaji katika shirika hilo kwa sababu faida itakayopatikana katika hisa inaweza kutumika katika shughuli za maendeleo. Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alipongeza mradi wa uzalishwaji wa mkaa mbadala wa kupikia kuwa utachochea utunzwaji wa mazingira kama Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 inavyoagiza.

Aidha, alishauri shirika hilo kuongeza uzalishaji wa mkaa huo ili uwafikie Watanzania wengi zaidi pamoja na kuangalia namna ya kuleta teknolojia ya kutengeneza mitambo ya kuchakata mkaa huo nchini ili kupunguza gharama za kuagiza kutoka nje.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika (PAPU), Dk. Sifundo Chief Moyo, alipofika Ikulu Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Mtuhumiwa 'panya road' adaiwa kuua mjomba, kunywa damu yake

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KIJANA Humphrey Shoo anayetuhumiwa kuwa sehemu ya wahalifu wa mitaani jijini Dar es Salaam 'panya road', anadaiwa kumuua mjomba wake, Godson Shoo (50), kwa kumchinja kwa panga na kisha kupiga magoti na kunywa damu yake.

Baada ya kunywa damu hiyo na kulishika koromeo kwa mkono, Humphrey alivamiwa na wananchi wenye hasira waliosikia kelele za Godson, akiomba msaada ili asiuawe.

Tukio hilo lilitokea Agosti 26 mwaka huu, saa tatu asubuhi katika Kitongoji cha Nkweshoo, Kijiji cha Mkuu Ndoo, Kata ya Machame Mashariki, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Simon Maigwa, jana alisema ana taarifa za Shoo kuuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali shingoni na mpwa wake, Humphrey.

"Chanzo cha tukio hili ni kitendo cha huyo kijana (Humphrey) kufika nyumbani kwa marehemu Godson na kumwambia ampe pesa (fedha).

"Mjomba wake alimwambia hana pesa, Humphrey akachomoa panga, akaanza kumfukuza na katika eneo la mita 150 wakati anakimbia, akaanguka, baada ya kuteleza, ndio akamkata.

"Wakati anakimbia alikuwa anapiga kelele kuomba msaada na wananchi waliokuwa karibu walivyosikia kelele wakamfuata kwa ajili ya kumsaidia.

"Kile kitendo cha kumkata na akanyonya damu yake, unaweza ukaona kwamba sio kitu cha kawaida. Kwa hiyo, kile kitendo kikatia watu hasira, wakajichukulia sheria mkononi, wakaanza kumshambulia kwa silaha za jadi.

"Na Jeshi la Polisi lilipopata taarifa lilikwenda na likamkuta Humprey, yuko kwenye hali mbaya na wakati wanamkimbiza kumpeleka Hospitali Teule ya Machame na yeye akapoteza maisha njiani,"alisema Kamanda Maigwa.

Akizungumzia tukio hilo kwa njia ya simu, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mkuu Ndoo, Twalib Mallya, alisema kijana huyo aliyemtuhumu kuwa alikuwa anajinasibu kijijini kuwa sehemu ya panya road jijini Dar es Salaam, alirejea kijijini huko wiki tatu zilizopita.

Mallya alisema: "Huyu jamaa (Humphrey) aliyeuawa na wananchi wenye hasira baada ya kumuua mjomba wake, ana wiki tatu hapa kijijini kwetu tangu arejee kutoka Dar es Salaam.

"Aliwahi kufanya matukio miaka mitano iliyopita, alivunja duka, akakimbia na stori zake alipokuja kijijini, anasema yeye ni kundi la panya road kule Dar es Salaam.

"Kutokana na vituko alivyokuwa akivifanya kijijini ilikuwa leo (Agosti 28), nimewaambia Mwenyekiti wa Kitongoji na wazee wengine, ilikuwa tumshike tumpeleke polisi."

Kwa mujibu wa Mallya, kitu kilichofanya amuue mjomba wake, ni pochi aliyoiona ikiwa na Sh. 40,000.


**UBALOZI WA SWEDEN, UINGEREZA, SWITZERLAND (HPSS PROJECT) NA WATAALAM MBALIMBALI DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Ubalozi wa Sweden, Uingereza, Switzerland (HPSS Project)** na Wataalam mbalimbali watauza kwa mnada wa hadhara Magari, Pikipiki, Generator na Fanicha tarehe 2 September, 2023 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fanicha zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa sets, Book case, Cabinets, Makabati, Meza za chakula, Viti, Meza za ofisi, Viti, Vitanda, Magodoro & Zanzibar bed, Fridge double door, Deep Freezer, Washer, Computer set, TV Set, Projector, Music systems, Nashuatec MP5002SP & MP6500 Photo copy m/c, A/C split units, Automatic Incubator, Solar system na vingine vingi.

**Magari,Pikipiki na Genereta yataanza kuuzwa Saa 6:00 mchana**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Toyota Land Cruiser Hard top | 1HZ Diesel Engine | 2016 | Bado |
| 2 | Nissan Patrol Station Wagon Y61 | TD42 Diesel & TGP Petrol | 2012 | Bado |
| 1 | Toyota Rov4 Station Wagon | 2AZ Petrol Engine | 2006 | Umelipwa |
| 1 | Komatsu Wheel Loader | W100 Diesel Engine | 1984 | Umelipwa |
| 1 | Ford Everest Station Wagon | WLAT Diesel Engine | 2004 | Umelipwa |
| 1 | Yamaha Motorcycle | 125 CC Petrol Engine | 2016 | Bado |
| 1 | Generator 165 KVA 3 Phase | Perkins Diesel Engine | 2015 | Umelipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 30 August mpaka 1 September 2023, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Genereta atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 8 September, 2023 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

# Mkakati wawekwa uzalishaji wa mpunga Afrika Mashariki, Kusini

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, amesisitiza azma ya Tanzania kuwa nguvu kuu katika uendelezaji wa kilimo cha mpunga kama moja ya mazao muhimu nchini.

Alitoa rai hiyo wakati akifungua mkutano wa siku tatu wa Washirika wa Uzalishaji wa Mpunga (RBI) kwa Afrika Mashariki na Kusini (ESA), uliojumuisha washiriki kutoka nchi 11, jijini Dar es Salaam.

Mweli alizungumzia umuhimu wa ushirikiano na wakulima, taasisi za utafiti, hasa TARI na mashirika ya kimataifa na kuisifu Taasisi ya Utafiti wa Mpunga ya Kimataifa (IRRI) kwa kazi inayofanya nchini.

"Serikali inapigania mabadiliko makubwa katika matumizi ya teknolojia ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mpunga kutoka chini ya tani 2.5 kwa hekta hadi tani tano au zaidi ifikapo mwaka 2030.

"Lengo letu kama serikali ni kuwa, Tanzania kuzalisha mpunga wa kutosha kukidhi mahitaji ya kitaifa, kuchangia katika kuimarisha usalama wa chakula kote Afrika na hatimaye kuwa mzalishaji wa mpunga namba moja barani," alisema.

Kadhalika, alisema programu ya RBI ni ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi uliolenga kukuza na kutumia aina bora za mpunga kwa wakulima wadogo katika ESA. Tanzania ina jukumu kubwa kama mzalishaji wa mpunga. Programu inatekelezwa na IRRI.

Mkutano huo umekusanya wataalam wa mpunga na wadau kutoka nchi 11, kila mmoja akiwa na lengo kuu la kuboresha uzalishaji wa mpunga katika eneo hilo.

Dk. Ajay Kohil, Mkurugenzi Mkuu wa IRRI, alisema mkakati wa kilimo wa Tanzania, kupitia Agenda 10-30, serikali imejiwekea lengo la ongezeko la asilimia 10 la uzalishaji wa mpunga ifikapo 2030.

Alisema dunia ina matarajio makubwa kwa Tanzania na nchi za ESA kuongeza uzalishaji wa mpunga, ambao bado ni tatizo kote duniani.

Mwakilishi wa Kikanda wa IRRI - Afrika, Dk. Abdelbagi Ismail, alisisitiza haja ya dharura ya Tanzania na nchi nyingine za ESA kuchochea maboresho katika uzalishaji wa mpunga ili kupambana na njaa na umaskini wa kipato kwa mamilioni ya wakulima wadogo.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema Tanzania ni mojawapo ya wazalishaji wakuu wa mpunga Afrika, lakini bado kuna nafasi kubwa ya kuboresha.

"Ninaamini pamoja tunaweza kutimiza mengi zaidi na kuleta tofauti ambayo hakuna mmoja wetu angeweza kufanya pekee yake. Tuendelee na ushirikiano huu mzuri na ukuaji," alisema Dk. Ismail.

"Tangu kuanzishwa kwake, IRRI imejitoa kuboresha programu ya mpunga Afrika, kuongeza uwezo wa washirika wetu na kuisaidia bara kufikia kujitosheleza kwa chakula tangu miaka ya 1960 mapema," alisema.

"Afrika ina asilimia 60 ya ardhi inayofaa kwa kilimo duniani ambayo haijatumika, lakini bado haiwezi kujilisha. Hii ni kwa sababu ya mavuno madogo, mazoea duni ya usimamizi wa shamba na soko la kilimo linalopotoshwa," alisisitiza Dk. Ismail.

Alisema SSA leo inaagiza chakula cha thamani ya dola bilioni 44 kila mwaka, na kati ya hizo, dola bilioni saba kwa mwaka kwa mpunga pekee, ambazo ni mzigo mkubwa kwa uchumi wa ndani.

"Nchi za SSA zinahitaji kuboresha uzalishaji wa ndani na ubora na kupunguza gharama za uzalishaji ili kuwa na bidhaa zinazoweza kushindana na kupunguza pengo la mahitaji ya ndani na pia kuongeza mapato kwa wakulima," alisema Dk. Ismail.

Alisema Tanzania inahitaji kufanya kazi kwa kuainisha sera na mwongozo wa kilimo; kuondoa vikwazo vilivyowekwa na nchi jirani ili kuruhusu biashara huru katika pembejeo za kilimo ikiwa ni pamoja na mbegu za aina bora, mbolea na kemikali nyingine za kilimo.

# Majiji kufungwa kamera za usalama

**Na Akida Akida**

SERIKALI katika kuendelea kuboresha utendaji wa Jeshi la Polisi kwenye kudhibiti matukio ya uhalifu na makosa ya usalama barabarani, imeamua kufunga kamera maalum katika majiji ya Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza na Arusha huku lengo likiwa kufunga kamera hizo katika mikoa yote nchini kwa siku zijazo.

Mpango huo ulibainishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, wakati wa mkutano wa kuwajengea uwezo wakuu wa mikoa yote na makatibu tawala uliofanyika katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere, kilichopo Kibaha mkoani Pwani.

"Katika kuimarisha utendaji kazi wa Jeshi letu la Polisi, kuna maeneo muhimu sana tumeamua kuyapa kipaumbele. Moja ni kujenga mazingira mazuri ya askari wetu kufanya shughuli zao ikiwamo makazi yao, vitendea kazi, matumizi ya mifumo na teknolojia za kisasa katika kubaini, kukabili, kushughulika na kudhibiti uhalifu.

"Nichukue fursa hii kuutambulisha kwenu mradi mkubwa wa Mji Salama. Kutokana na juhudi za Mheshimiwa Rais kuimarisha demokrasia ya uchumi, tumeweza kupata mkopo wenye masharti nafuu unakuja kutusaidia kusimika mradi wa kimkakati wa mji salama," alisema Waziri Masauni.

"Miji ambayo tutaanza nayo ni Mji wa Kibiashara Dar es Salaam, Makao Makuu ya Nchi-Dodoma, Makao Makuu ya Utalii - Arusha pamoja na Jiji la Mwanza huku mradi huo ukienda sambamba na Mradi wa Ukaguzi wa Lazima wa Magari na Mradi wa Bwalo la Maofisa wa Polisi Dar es Salaam," aliongeza.

Waziri Masauni katika mkutano huo alitaja maeneo mengine ya vipaumbele kwa Jeshi la Polisi ambayo yashaanza kufanyiwa kazi ni pamoja na kuendelea kudumisha usalama wa raia na mali zao kwa kufanya doria, misako na operesheni maalum katika mipaka, maziwa makuu na bahari ili kudhibiti uhalifu nchini na kupunguza matishio ya uhalifu, makosa makubwa ya jinai na ajali za barabarani.

Alitaka jamii kuendelea kushirikishwa katika masuala ya ulinzi kupitia kitengo cha polisi jamii, kuimarisha weledi wa maofisa, wakaguzi na askari kupitia mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi sambamba na kuhudhuria mikutano ya kanda, kikanda, kimataifa na operesheni za kimataifa ili kuboresha huduma za polisi nchini.

The Guardian Limited

JOB VACANCY

The Guardian Limited, **Publishers of leading Tanzanian newspapers, The Guardian, Nipashe and Nipashe Jumapili, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

**SENIOR MARKETING EXECUTIVE – DAR ES SALAAM**

**Job Purpose:**

Developing and executing strategies to promote brands, products and services, maximizing profits for the company.

**Main Responsibilities:**

- Formulate an appropriate commercial strategy that responds to the overall development of the company's marketing operations, newspaper sales, advertisements and other printed products.
- Become knowledgeable expert of The Guardian Limited products and be experienced in identifying target markets and developing strategies to communicate with them.
- Identify, plan, prepare and produce proposals for the targeted audiences.
- Study competitors' products and services on a daily basis, with a view to designing counter strategies.
- Advise clients on their advertising and promotion campaigns.
- Organize all company events related to CSR, promotion, product launching, staff parties, etc.
- Monitor and analyze product performances, trends and provide accurate reports on programe and market information.
- Explore ways of improving existing products and services and increasing profitability.
- Advise the Management with feasibility studies on ways to get sponsorship for various events, highlighting benefits to the Company.
- Engage in negotiating and closing deals where and if appropriate.
- Prepare periodic performance reports for the Management and provide appropriate inputs towards improvement and the taking of remedial measures.
- Design and implement human resources training and development programme

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 5 years' relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge and familiarity with a wide range of newspaper brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via email address: **vacancy@guardian.co.tz** by **8th September, 2023.**

**NB:** Only shortlisted candidates will be contacted.

***Please note that The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

HABARI KITAIFA

# Wanaotumia Flagyl kuzuia ujauzito wapewa angalizo

**Na Christina Mwakangale**

MABINTI wamehadharishwa dhidi ya matumizi holela ya dawa ya Flagyl wanayodaiwa kuitumia kuzuia ujauzito.

Inadaiwa baadhi yao hununua na kujipangia wao wenyewe namna ya kuzitumia, hata kumeza vidonge tisa ndani ya saa chache, wakionywa madhara yake ni pamoja na kuathiri uoni na husababisha mwili kufaganzi.

Daktari Bingwa wa Uzazi katika Idara ya Uzazi Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala (MRRH), Mugalu Kitandu, alitoa angalizo hilo wiki iliyopita wakati wa mafunzo ya Tanzania Media Foundation (TMF) mkoani Dar es Salaam yaliyolenga kuhamasisha vyombo vya habari kujikita katika uandishi wa habari za afya ya uzazi na uzazi wa mpango .

Alisema kwa sasa kumekuwa na ongezeko la matumizi holela ya dawa hiyo, hasa kwa mabinti waliopo masomoni, wakinunua katika maduka ya dawa Flagyl, bila mwongozo wa wataalamu wa afya, kisha kuzimeza kwa lengo la kuzuia kupata ujauzito.

"Mbali na matumizi ya P2 kuwa makubwa kama ambavyo hata Waziri wa Afya amekemea matumizi hayo ya dawa hiyo ambayo ni maalum kwa ajili ya matumizi ya dharura, sasa hivi wasichana wanatumia dawa ya Fragyl wakidai baada au kabla ya tendo la ndoa ni kinga dhidi ya mimba, inasafisha kizazi.

"Kuna haja ya kuongeza wigo wa elimu ya afya ya uzazi na taarifa sahihi kuhusu afya ya uzazi, ili vijana hawa wajue watumie ipi. Kwa sababu kiuhalisia mabinti waliopo vyuoni, hata shuleni, hasa za sekondari wanajihusisha na ngono, tena na vijana wenzao. Matokeo yake mimba, utoaji mimba holela na kuhatarisha uhai," alisema Dk. Mugalu.

Ofisa Afya Mwandamizi anayeshughulikia Idadi ya Watu - Shirika la Pathfinder, Dk. Samuel Kikaro, alisema dhana iliyoko miongoni mwa vijana hasa walioko masomoni ni kuogopa mimba, hivyo baadhi hudiriki kutumia mbinu tofauti kuzuia, zikiwamo zisizo za kitaalamu.

"Hivi sasa mabinti wanaogopa mimba, yaani watoto wanaogopa mimba kuliko Ukimwi. Kwenye njia za uzazi wa mpango, kuna minong'ono mingi, imani potofu, tamaduni za kiafrika kwamba zinaathari, lakini ukweli ni kwamba vijana wetu, tena wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 24, baadhi wanashiriki ngono.

"Ipo haja ya kuongeza elimu ya afya ya uzazi, kwa sababu takwimu za kitabibu zinasema mimba chini ya miaka 20 ni hatarishi, pia asilimia 25 ya walio katika umri wa kuzaa nchini, wanahitaji huduma ya afya ya uzazi ila hawafikiwi na huduma," alisema Kikaro.

TMF imekuwa inaita wataalamu wa maeneo mbalimbali kuzungumza na waandishi wa habari kwa lengo la kubainisha maeneo yanayopaswa kumulikwa na vyombo vya habari na kuzalisha habari/ripoti za uchunguzi na uwajibikaji.

# Kicheko watumishi wa umma wakipokea nyongeza mshahara

**Na Halfani Chusi**

WATUMISHI wa umma wameipongeza serikali kwa kutimiza ahadi ya nyongeza ya mshahara, wakisisitiza kufanya hivyo kila mwaka wa fedha kwa mujibu wa sheria.

Ni pongezi walizozitoa katika mazungumzo na Nipashe kwa nyakati tofauti kuhusu nyongeza ya mshahara kama ilivyoahidiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, wakati wa sherehe za Mei Mosi mwaka huu, wakithibitisha kupata nyongeza hiyo.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Mgowelo, wilayani Kilolo, mkoani Iringa, Victor Kalinga, alisema ameona ongezeko la mshahara wake mwezi huu katika akaunti yake. Alisema ongezeko limeongeza motisha ya kazi.

"Nimeona ongezeko kwenye mshahara wangu, japo ni kidogo, lakini siyo mbaya. Angalau kuna kitu kimefanyika kwenye kipato changu.

"Ninashukuru kwa hatua hiyo. Ninaiomba serikali iendelee kuboresha mambo mengine yanayowahusu watumishi wa serikali, ili wafanye kazi kwa ubora, ubunifu, ufanisi na tija," alishauri Mwalimu Kalinga.

Mtumishi mwingine toka sekta ya afya, Happy Daniel, alisema imekuwa furaha kwake kuona nyongeza ya mshahara, akikumbushia kuwa jambo hilo lilikuwa halijafanywa kwa muda mrefu.

Alisema Rais Samia alipoahidi kuongeza ujira, aliona kama ndoto, "Mwezi uliopita (Julai) tulipoona hakuna ongezeko, nilijua imeshindikana, lakini mwezi huu tumeona ongezeko ambalo ni la mwezi uliopita na huu.

"Nimefurahia nyongeza hii. Imekuja kwa kiwango tofauti tofauti kwa kila mtumishi kutokana na nafasi yake pamoja na kiwango cha mshahara. Kwa wale wanaoona kama imekuja kidogo, yawezekana pengine mshahara wake mdogo," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema ongezeko hilo ni kwa watumishi wote wa serikali. Hakuna aliyerukwa.

"Tumetimiza ahadi, mwezi uliopita hawakuona ongezeko na tuliahidi watajumlishiwa kwenye mshahara wa mwezi huu," alisema Simbachawene.

Akiwa kwenye sherehe za Mei Mosi mwaka huu, Rais Samia aliahidi kuongeza mishahara kwa wafanyakazi, akitamka "kuna nyongeza za mshahara za kila mwaka ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zimesitishwa, nikaona mwaka huu tuzirudishe.

"Kwa hiyo, wafanyakazi wote niseme kutakuwa na nyongeza ya mishahara ya kila mwaka. Tutaanza mwaka huu na tutakwenda nalo kila mwaka."

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## LIMERUDIWA: MAOMBI YA KUONYESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA ZA MAFUTA KWA MAGARI MDOGO NA VIFAA VINGINE KWENYE NJIA YA MKUZA WA BOMBA LA MAFUTA KATIKA MRADI WA EACOP. KUMBUKUMBU Na. 00000315

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD"), inaalika kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya mafuta kwa ajili ya magari madogo na vifaa vingine kwenye njia ya Mkuza nchini Tanzania.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili, kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale, katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
EACOP Ltd, ina Magari/mitambo, kadhaa ambayo hufanya kazi mbalimbali kwenye maeneo yashughuli za EACOP na hivyo magari hayo yatasambazwa kote chini Tanzania. Magari na mitambo hiyo yote itahitaji kuwekewa mafuta katika vituo mbalimbali ndani na nje ya maeneo ya uendeshaji wa mradi. Kwa hiyo, EACOP Ltd inahitaji watoa huduma mbalimbali kueleza nia yao ya kutoa huduma za mafuta kwa Kampuni ikiwa ni pamoja na usambazaji wa:

- Mafuta ya Petroli na Dezeli.
- Huduma nyingine zinazohusiana na magari na mitambo midogo ikijumuisha, huduma ya kuosha magari katika vituo hivyo vya mafuta, na/au uwezo wa kutoa huduma ya Oili, grisi, na huduma za ndogo zisizo za kimakanika.
- Kwa sasa Mradi unapitia katika mikoa ya Bukoba, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga hususan katika wilaya za Muheza, Handeni, Kilindi DC, Kibirashi, Kiteto (Kibaya), Hanang, Chemba, Igunga, Kagongwa, Bukombe (Ushirombo), Chato, Muleba, Misenyi (Mutukula), Kyaka kwa hiyo mtoa huduma lazima awe na kutuo cha mafuta katika maeneo hayo na Tanzania kwa Ujumla.
- Inapendekezwa sana kituo cha mafuta kiwe na Kadi za usumaku za kukwaruza au zenye msimbo na nywira au namba za siri za kutolea mafuta.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Kampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo.**

- Uthibitisho wa kusajiliwa kama muuzaji wa mafuta/Kituo cha mafuta/Kampuni ya mafuta kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na mamlaka husika ikiwa ni pamoja na OSHA, EWURA, TBS etc.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kufanya kazi katika miradi yenye mahitaji makubwa ya mafuta ikijumuisha orodha ya kampuni 5 unazofanya nayo kazi kwa sasa au yaliyopita.
- Leseni ya Biashara.
- Cheti cha usajili toka BRELA (ambatanisha cheti).
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlakaya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha mlipa kodi cha mwaka wahivi karibuni.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya ndani.
- Ushahidi wa sera na Mifumo ya Usimamizi wa shirika la HSE, utaratibu na mchakato kwa mujibu wa viwango vinavyotumika vya ndani na Viwanda kwa kazi zinazofanana.
- Uthibitisha wa wasifu wa wafanyakazi mhimu watakaohusika katika kutoa huduma za mradi ikijumuisha vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma husika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha ya miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho wa kupiga vita rushwa, ufisadi, kwa kuzingatia Haki za Binandamu.

Kampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu zinakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**). Maombi yatumwe kabla au mnamo tarehe **12 Septemba 2023 saa 11 jioni** saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000195 - kutoa huduma ya Bima ya Dhima kwa wakurugenzi na Mafisa wa Mradi wa EACOP**. Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.
Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni zitakazojumuishwa kwenye orodha ya (kampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Kampuni zilizofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

29 17574102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# STAMICO ni mfano wa kuigwa kwa mashirika ya umma

**SHIRIKA** la Madini la Taifa (STAMICO) ni mfano wa kuigwa kwa mashirika ya umma baada ya kutoka kwenye hali ya kujikongoja hadi sasa kufikia hatua ya kutoa gawio kwa serikali.

Shirika hilo lililoanzishwa mwaka 1972 sasa linatimiza miaka 50 likiwa limepitia misukosuko ya kujikongoja hadi sasa kusimama imara na kuweza kujiendesha.

Lilianzishwa kwa lengo la kuwekeza kimkakati katika miradi ya madini na uvunaji wa rasilimali madini kwa niaba ya Umma kwenye mnyororo wote, kuanzia uchimbaji hadi kufika sokoni.

Kama yalivyo mashirika mengi ya serikali kutegemea ruzuku kutoka serikalini ili yaweze kujiendesha, hivyo ndivyo lilivyokuwa Shirika la STAMICO.

Lilikuwa likipata ruzuku kutoka serikalini ya Sh. bilioni 3.4 huku likikusanya mapato ya ndani ya Sh. bilioni 1.3 na hivyo kusababisha hasara.

Lakini kwa sasa Shirika hilo linakusanya mapato ya ndani ya Sh. bilioni 61. 1 na kuwa Shirika lililotoka kutengeneza hasara hadi kufikia linalotengeneza faida.

Shirika hilo limeweza kulipa gawio serikalini la jumla ya Shilingi bilioni nane na kuondokana kabisa na utegemezi wa ruzuku na hadi kupata hati safi kwa miaka mitatu mfululizo kutokana na ukaguzi wa mahesabu.

Mafanikio yote hayo yametokana na miradi mbalimbali iliyoanzishwa na pia shirika kufanyiwa marekebisho ikiwamo wa kimuundo na kimajukumu.

Katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2019 shirika limefanya mageuzi makubwa na kufanya kuwa chombo madhubuti katika sekta ya madini.

Tunasema kama hili limeweza kufanyika kwa STAMICO linawezekana pia kwa mashirika mengine kuiga mfano huo ili na yenyewe yaweze kubadilika.

Mashirika mengi yamekuwa yakijiendesha kihasara kwa sababu ya kung'ang'ania mfumo uleule ulioanzishwa nao ndio maana serikali inaendelea kupata hasara kwa kuendelea kuyapa ruzuku ili yaweze kujiendesha.

STAMICO kwa sasa imedhamiria kujitoa kwenye utegemezi wa ruzuku ya mishahara kutoka serikalini na kuanza kujilipa yenyewe.

Haya ni mafanikio makubwa ambayo yanapasawa kuwa mfano kwa mashirika mengine ya serikali.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse, siri ya mafanikio hayo ni kubadilika kimtazamo, akimaanisha kwenda na mabadiliko yanayotokea duniani na vilevile kuzingatia nidhamu kwenye utekelezaji majukumu. Hii ni pamoja na kuzingatia muda uliopangwa kutekeleza jambo fulani ufanyike kama ulivyopangwa na kwa kuzingatia muda mliojiwekea.

Vilevile, kwenye mipango ni lazima inapopangwa itekelezwe kwa pamoja na wafanyakazi wote bila kuwa na ubinafsi wala makundi.

STAMICO ina mipango mingi ya baadaye ikiwamo kutekeleza mafunzo kwa ajili ya kutoa elimu kwa wachimbaji mikoa yote nchini, kuongeza uwezo wa vituo vya mfano na kuendeleza ujenzi wa vituo vipya vya Lindi na Tanga, kuwasaidia kupata vifaa, mitaji na kuwaunganisha na wadau husika na kufanikisha uanzishwaji wa benki ya wachimbaji nchini.

Kwa mipango hii tunaiona STAMICO ikipiga maendeleo makubwa na hata kuwa shirika linalofanya vizuri zaidi nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Vijana wasiachiwe kuhatarisha amani

Na Tuntule Swebe

**KATIKA** miji mingi kumesikika taarifa za vijana wanaojiingiza kwenye kuvuta bangi na kufanya uhalifu ukiwamo kupora watu, kutishia amani, kuvamia nyumba, kujeruhi na hata kuua wakijibandika majina mathalani, panyarodi.

Hali hii imesababisha wananchi wawe wanyonge na hata wenye vipato vikubwa kuishi kwa hofu na kujiona kuwa maisha yanakwama kutokana na kuongezeka uhalifu kwenye maeneo yao.

Pengine tutajiuliza chanzo ni nini? Nionavyo mimi shida inaanzia kwenye familia wazazi na walezi kutokuwa makini kuangalia watoto wao kisa wanadai kuwa na majukumu mengi kupambana ili maisha yasonge bila kujua watoto wakoje walikuwa wapi, wameingia ndani sa ngapi na kipi walichofanya.

Mambo hayo yamesababisha watoto kujiunga na makundi ya wahalifu ya wavuta bangi, walevi, watumia dawa za kulevya na wakabaji na hata wezi.

Watoto kukimbia nyumbani na kwenda kushinda mitaani hali hii inasababisha wengine kujifunza na kujiunga na makundi maovu. Suala la watoto yatima ambao wazazi wao wamefariki nalo husababisha kukosa mwelekeo na kuingia mitaani kujiunga na makundi ya watukutu.

Kuna baadhi wanatoka vijijini wakikimbilia mijini wakiamini huko kuna maisha bora na fedha inapatikana kwa urahisi, hivyo hukimbilia mijini bila kuwa na mahali pakufikia, wanapofika hukaribishwa na makundi mbalimbali ya watoto wanaoishi mitaani kama panyarodi na hivyo kujiunga nao kwenye uhalifu.

Wakati mwingine chanzo ni hulka au tabia zao wenyewe vijana kwani hupenda kujaribu au kuiga na wengine wanaweza kuwa wanakwama maisha kutokana na uvivu na kutojituma kwenye kazi.

Maeneo ya Boko Basihaya wakazi wa maeneo hayo wanauhusisha ongezeko la vijana kwenye uporaji na kuwa na uelewa mdogo wa mambo mengi na kukosa ubunifu wa mambo mbalimbali katika kutafuta pesa.

Wengi wanatamani kuwa na fedha lakini uwezo wao ni mdogo lakini kazi kama vile kuuza mahindi, viatu, kuwa kakalishe kunawashinda kutokana na kukosa ubunifu. Ukweli ni kwamba kuna biashara nyingi zinazotumiwa kuongeza kipato ila wao badala ya kuona kuwa ni kitu cha kufanya wanatamani urahisi ikiwa ni pamoja na kuwaibia watu na wakati mwingine kuwadhulumu.

Je, waungwana watajiuliza nini kifanyike ili tuweze kukomesha kundi hili la watoto na vijana wasumbufu kwenye jamii?

Kuna maelezo kuwa nyuma ya vijana hawa wakati mwingine kuna vigogo wanaowatumia kama vibarua na kujinufaisha wenyewe.

Yapo madai ya wafanyabiashara wengine kuwatumia na kuwapa pesa ya kula au kidogo wakati wao wakichukua vitu walivyovipora kwa maslahi yao binafsi na kuendelea kuhatarisha maisha ya vijana hao bila kujali.

Wakati umefika wazazi na walezi kuwaelimisha watoto na vijana wao juu ya wimbi la kujiingiza kwenye maisha ya kihalifu na wizi ikiwamo kujiunga na makundi kama panyarodi na kulichukulia suala hilo kama wajibu wao. Wakiwaelekeza na kuwafundisha maadili mema kwa kuwa asiyefunzwa na wazazi au walezi atafunzwa na dunia.

Mara nyingi mafunzo ya dunia ni kuuawa, kujeruhiwa na wakati mwingine kupata ulemavu wa kudumu.

Pamoja na malezi, vikosi vya ulinzi shirikishi ambao ni watu walio katika mitaa wawe bega kwa bega na serikali zao za mitaa kutoa taarifa, kuonya, kufuatilia watuhumiwa ili kupambana kutokomeza mienendo hiyo.

Aidha, ni vyema kuwe na semina au mafunzo ya mara kwa mara kwa vijana zinazohusu maendeleo yao, mbinu na mikakati ya kujenga maisha yao na kupambana ili kuwekeza kibiashara kuwawezesha kukabiliana na umaskini na uhalifu.

Hali kadhalika serikali itunge sheria na kutoa adhabu kwa vijana wanaoshiriki makundi haya na hata kwa hao vigogo wanaowatuma ili kufanya uhalifu.

HABARI KITAIFA

## Wanawake, wasichana watakiwa kuchangamkia fursa kiuchumi

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Adolf Ndunguru, amewahamasisha wanawake kuchangamkia fursa zinazotolewa na mradi wa uwezeshaji wanawake na wasichana kiuchumi na uongozi (WLER), unaotekelezwa na UN Women, ili kupata maarifa na ujuzi utakaochangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya nchi.

Aliyasema hayo hivi karibuni wakati akifungua Kikao cha Kamati ya Uongozi WLER kilichofanyika kwa siku mbili, mkoani Mtwara, ukiwa ni miongoni mwa mikoa sita mradi unaotekelezwa chini ya ufadhili wa serikali ya Finland.

Mradi huo ulianzishwa mwaka 2022, unatekelezwa kwa miaka minne katika mikoa ya Lindi, Arusha, Singida, Pwani na Dar es Salaam.

Mwakilishi wa UN Women Nchini, Hodan Addou, alisema mradi unajitahidi kuchangia matokeo bora ya maendeleo ndani ya mikoa na taifa kwa ujumla kupitia kushiriki mafunzo.

"Mradi wa WLER unafanya kazi ya kukuza sauti ya wanawake na kuendeleza haki za kiuchumi za wanawake kupitia hatua kama vile kukuza kanuni za mwitikio wa kijinsia na kuleta mabadiliko ya kizazi chenye usawa," alisema.

Alisema takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, ni asilimia 3.4 tu ya wanawake wanaomiliki wa ardhi.

Alisema moja ya hatua muhimu za mradi huo katika wilaya ni kuongeza uelewa kwa wanawake katika jamii kuhusu umuhimu wa kuwa na hati miliki rasmi ya ardhi, ambayo itawapa usalama na kuboresha upatikanaji wao wa mikopo.

"Wanawake wengi ama hawajui kwamba ardhi inaweza kusajiliwa na hati miliki zinaweza kupatikana

na kurahisisha upatikanaji wa mikopo ili kuimarisha biashara zao," alisema Juliana Manyama, Ofisa Maendeleo ya Jamii.

Alisema kupitia mradi huo, wamebaini wanawake 465 wa Mtwara-Mikindani Manispaa ambao wanamiliki sehemu za ardhi bila ya kuwa na hati.

Mkuu wa Ushirikiano wa Ubalozi wa Finland, Juhana Lehtinen, alisema: "Nimefurahi kuona kwamba uongozi wa juu wa Serikali ya Tanzania umejitolea kukuza usawa wa kijinsia na uongozi wa wanawake. Kwa upande wa programu hii, tunaweza kusema kweli kwamba malengo ya mpango yanalingana kikweli na sera na malengo ya kitaifa. Hii ni fursa nzuri kwa programu kufanya kwa njia bora na kufikia matokeo mazuri."

Aliipongeza timu ya UN Women na Serikali ya Tanzania kwa matokeo mazuri yaliyopatikana hadi sasa.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wakili Amon Mpanjo, alisema mradi huo ni chombo muhimu cha kuwawezesha wanawake nchini.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Makatibu Wakuu kutoka TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

Wengine ni Makatibu Tawala wa Mikoa, Maofisa Maendeleo ya Jamii kutoka kanda sita za mradi, Ubalozi wa Finland, asasi za kiraia, asasi za wanawake wenye ulemavu ambao kwa pamoja walitafakari maendeleo ya mradi na kupanga njia ya utekelezaji wake kwa ufanisi.



Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Rajab Yussuf Mkasaba, akitoa msaada wa vyakula kwa niaba ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa wazee na yatima wa Shehia za Muyuni A, B, C zote 21 za Wilaya ya Kusini Unguja, ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za Wiki ya Tamasha la Kizimkazi ambalo Rais Samia ndiye mwasisi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia kuzindua shule mbili Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuzindua Shule ya Msingi na Sekondari ya Kizimkazi zilizopo Mkoa wa Kusini Unguja zilizokarabatiwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Uzinduzi huo unatarajiwa kufanyika leo mjini Unguja, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra ya Tamasha la Sherehe za Kizimkazi na ukarabati huo umeenda sambamba na uboreshaji wa ofisi za walimu na maabara, matundu ya vyoo 14, ukumbi wa mikutano kwa Sh. milioni 277.

Akizungumza na waandishi wa visiwani Zanzibar, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Islam Seif Salum, alisema shughuli ya ujenzi wa shule hizo umemalizika na kilichobaki ni kuweka madawati, meza na viti.

"Tunasubiri kwa hamu Kizimkazi tuonyeshe maendeleo yetu hii TASAF pamoja na kusaidia kaya maskini lakini inashughulika na uboreshaji wa miundombinu ya shule na hospitali," alisema Dk. Salum. Kaimu Mkurugenzi wa TASAF, Shadrack Mziray alisema wanatekeleza majukumu Tanzania Bara na Visiwani, kwamba kumekuwa na maendeleo ya ukarabati wa Shule ya Kizimkazi.

Alisema ujenzi na ukarabati wa shule hizo ulipaswa kukamilika kipindi cha mwaka mmoja, lakini mafundi wametumia muda wa miezi sita kukamilisha.

Alisema: "Ukizungumzia TASAF watu wanajua inafanya jambo moja la kuziwezesha kaya maskini kwa kuzipa ruzuku, bali tunatekeleza majukumu pia ya kutoa ajira za muda sambamba na kuboresha miundombinu".

Mkurugenzi wa Uratibu wa Shughuli za Serikali kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar Siajabu Suleiman Pandu alisema kumekuwa na utofauti mkubwa wa mwonekano wa Shule ya Kizimkazi baada ya kufanyiwa maboresho makubwa ya miundombinu.

Alisema: "Tunaishukuru TASAF wametoa fedha kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hii, kilichobaki ni taratibu ndogondogo ikiwamo usafi kabla ya mwenye jambo lake (Rais Samia) kuja kutembelea. Wananchi wawe watulivu na kumsubiri mama yetu (Rais Samia) ambaye atakuwa sehemu ya baraka ya tukio hili".

Tamasha la Kizimkazi lilianzishwa Agosti mwaka 2015 likitambulika kwa jina la Samia day kabla ya kubadilishwa jina mwaka 2018 na kuitwa Kizimkazi Day.

Lengo la tamasha hilo ni kutangaza utamaduni, vivutio na rasilimali za Kizimkazi mbapo hufanyika Agosti ya kila mwaka.


MEDIA COUNCIL OF TANZANIA

**NOTICE**
**FOR CONVENING OF THE 25TH NATIONAL GENERAL CONVENTION**

The President of the Media Council of Tanzania (MCT) hereby notifies MCT members, in accordance with Article 13 of the MCT Constitution, that the 25th National General Convention (NGC) of the Media Council of Tanzania will be held in Arusha on September 28, 2023. The venue and time of the meeting will be communicated in due course.

THE PROPOSED AGENDA AT THE 25TH NGC IS AS FOLLOWS:

1. Opening;
2. Adoption of Agenda;
3. Confirming Minutes of the 24th National General Convention held at Dodoma Rock Hotel, Dodoma on September 28, 2022;
4. Matters arising from the 24th NGC;
5. Report of the Executive Secretary;
6. Adoption of 2022 Audited Financial Statements;
7. Appointment of External Auditor for the period ending December 31, 2023;
8. Governing Board Election;
9. A.O.B;
10. Closing.

MCT members who have not paid their annual subscription fees by the deadline are reminded to do so immediately.

Judge Juxon I. Mlay
President
Media Council of Tanzania (MCT)

21757440?

# Kamati ya Bunge yataka DART iongeze mabasi kwa ubia

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Bunge ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa (TAMISEMI) imeagiza Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uendeshaji wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) na kuongeza idadi ya mabasi ili kurahisisha usafiri huo wa haraka.

Maagizo hayo yalitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Justine Lazaro, wakati wa majumuisho ya ziara ya wajumbe wa kamati hiyo waliotembelea mradi wa BRT awamu ya tatu.

Awamu ya tatu ya mradi huo itakayoanzia katikati ya Jiji kuelekea Gongo la Mboto inatarajiwa kukamilika mwezi Machi mwakani.

"Tumeona maendeleo ya ujenzi wa miundombinu mko vizuri, lakini hii kasi iende sanjari na kuongeza idadi ya mabasi yatakayotoa huduma na shirikisheni sekta binafsi.

"Ninyi DART mmiliki miundombinu, lakini uendeshaji mabasi wawe sekta binafsi ili tupate mabasi ya kutosha," alisema.

Alinainisha ni muda mwafaka kuhakikisha teknolojia ya smart card inaanza kutumika ili abiria wasipate kero wanayoipata wakati wa kukata tiketi.

"Miundombinu kama hii inapojengwa basi kuwe na uharaka wa kuweka mifumo ya kisasa ya ukusanyaji wa mapato na tumefurahi kuona mnatumia wataalamu wa ndani, lakini hakikisheni mifumo yetu hii ya kisasa haiharibiwi.

"Naamini kwamba mmejipanga vyema na hawa wanaofanya kazi hii wataendelea kuifanya kwa uzalendo mkubwa," alisema.

Alimpongeza Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Edwin Mhede na watumishi wa wakala kwa namna wanavyosimamia miradi hiyo kwa weledi mkubwa.

Aliitaka DART kuwa na mifumo mbadala ya kusanyaji mapato badala ya kutegemea mfumo mmoja ambao unapoharibika unaweza kusababisha taharuki na watu kushindwa kutumia usafiri huo.

"Kama mfumo mmoja haufanyi kazi, basi kuwe na njia nyingine ya kufanya shughuli ziendelee kama kawaida. Tuna uzoefu kwenye baadhi ya maeneo watu wanatengeneza mfumo mmoja ukisimama na huduma, zinasimama sasa mfumo wenu ukisimama mtasababisha taharuki kubwa sana," alisema

Mtendaji Mkuu wa DART, Edwin Mhede, alisema mkandarasi anayejenga mradi wa BRT awamu ya tatu amefikisha asilimia 17.5 ya ujenzi ingawa kwa mujibu wa mkataba alipaswa kuwa amefikia asilimia 29.5 kwa sasa.

Alisema kwa kushirikiana na wadau kwenye mradi huo ambao ni Mkandarasi Mshauri, Wakala wa Barabara (TANROADS), Mhandisi mwelekezi pamoja na kuchelewa huko lazima akamilishe mradi huo ifikapo mwezi Machi mwaka 2024.

"Ili kukamilisha mradi huo kwa wakati tumekubaliana kwamba tunaongeza nguvu kazi na saa za kufanya kazi yaani badala ya kufanya kazi saa nane sasa watafanya kazi usiku na mchana kwa hiyo tunaamini kwamba mradi utakamilika kwa wakati uliopangwa na hakutakuwa na muda wa nyongeza," alisema.

Aliongeza kuwa wabunge wameiagiza DART kutambua mchango wa wazawa wanaoshiriki kwenye ujenzi wa mradi huo na kuwapa vyeti wanapokamilisha mradi ili iwe rahisi kwao kupata kazi kwenye kampuni mbalimbali za ujenzi.

"Wabunge wametushauri kwamba watu wetu walioshiriki kusanifu mfumo wa BRT, mfumo wa kielektroniki wa kukusanya nauli na kwenye ujenzi wa miundombinu yenyewe ya barabara tuwatambue kwa hiyo tunajiandaa kuwatambua kwa njia iliyo rasmi," alisema Dk. Mhede.

Kuhusu kushirikisha sekta binafsi kama wabunge walivyoshauri, Dk. Mhede alisema hivi sasa wako kwenye hatua mbalimbali za ununuzi wa mabasi hayo kwa kushirikisha sekta binafsi.

"Kwa kadri kasi ya ujenzi wa miundombinu ya BRT inavyoongezeka na sisi tunajipanga kwenye ununuzi wa mabasi ili barabara zikikamilika tu mabasi yaanze kazi mara moja, hatutaki barabara ikamilike halafu mabasi hakuna au mabasi yafike kwanza barabara hazijakamilika," alisema.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima akizungumza katika kikao cha wadau wa kupambana na ukatili wa jinsia jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na kutangaza kuanza kwa tamasha liitwalo Zijue 'Fursa, Imarisha Uchumi, Kataa Ukatili, Kazi Iendelee nchi nzima'. Kulia ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Mabalozi wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia (FAGDI), Saimon Mpagatwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Jinsia katika wizara hiyo, Juliana Kibonde. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Waomba kujengewa bweni kukabili changamoto kukosa vipindi shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Mbwawa Miswe, wilayani Kibaha, mkoani Pwani, wameomba kujengewa bweni katika shule yao ili kuondokana na tatizo la baadhi yao kukosa vipindi vya masomo kwa kushindwa kuvuka Mto Ruvu wakati wa mvua.

Katika eneo hilo wanafunzi wamekuwa wakishindwa kuvuka Mto Ruvu kwa wakati, nyakati za asubuhi hasa wanapokuta mtumbwi ukiwa upande wa pili majira ya asubuhi na kipindi cha mvua maji yanapokuwa mengi na hivyo kulazimika kubaki nyumbani.

Rehema Yassin, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule hiyo, alisema juzi kuwa wanafunzi wanaoishi na wazazi wao upande wa pili wa Mto Ruvu, wamekuwa wakikosa masomo mara kwa mara kutokana na ukosefu wa kivuko, hivyo endapo kutakuwa na bweni litaondoa kikwazo hicho.

"Kuna uhitaji wa bweni kutunusuru kukosa vipindi na pia vishawishi kwa sisi watoto wa kike ambao tunatembea umbali mrefu kuja shuleni na kurudi nyumbani. Tunaomba pia kupata taulo za kike, baadhi yetu wanapokuwa kwenye siku zao wanashindwa kuja shuleni," alisema

Ezekiel Bashir, mwanafunzi wa kidato cha nne shuleni huko, alisema baadhi ya wanafunzi wanaoishi mbali na shule, wamekuwa wanakumbana na vikwazo kwenye usafiri kwa baadhi ya vyombo vya usafiri kushindwa kuwachukua kutokana na nauli zao na hivyo kuchelewa vipindi vya masomo. Mkuu wa Shule hiyo, Getrude Hamaro alisema ukosefu wa bweni katika shule unasababisha wanafunzi wanaoishi umbali wa kilomita sita mpaka nane kuchelewa kufika darasani huku wanaoishi ng'ambo ya Mto Ruvu, wakati wa masika wanashindwa kuvuka kutokana na kukosekana kivuko.

Alimshukuru Diwani wa Mbwawa, Judith Muluge kwa jitihada za kutafuta wafadhili kwa ajili ya ujenzi wa bweni litakalowanusuru wanafunzi, hususani wa kike.

Diwani wa Mbwawa, Judith, alisema aliamua kuwatafuta wafadhili Rehema Foundation ili kusaidia ujenzi wa mabweni katika kata hiyo na kata nyingine za Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Sifa Mwami, mmoja wa wakazi wa Mbwawa, alisema kujengewa bweni kutasaidia wanafunzi kupata muda mwingi wa kujisomea wakiwa shuleni.

# W'biashara Soko la Kariakoo kuwa na bima

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI iko katika mazungumzo na taasisi za fedha ili kuwawezesha wafanyabiashara wote 2,400 watakaoingia Soko la Kariakoo kuanzia Novemba mwaka huu kuwa na bima ya biashara zao.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Meneja Mkuu wa Soko la Kariakoo, Valentine Kaijage, alipotoa taarifa kwa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliyotembelea soko hilo mwishoni mwa wiki.

Alisema wakati soko linaungua ni wafanyabiashara sita tu waliokuwa wamekatia bima biashara zao, lakini wengi hawakuwa na bima ya aina yoyote na kati ya hao sita ni mmoja tu aliyetimiza vigezo vya kulipwa fidia na benki alikokuwa amekata bima hiyo.

"Tumejipanga na tumezungumza na benki na taasisi mbalimbali za fedha ziko tayari kusaidia mpango huu wa bima kwa wafanyabiashara tunaendelea kuzungumza nao," alisema.

Alibainisha kuwa jitihada zinafanywa na uongozi wa soko hilo kuwapa elimu wafanyabiashara watakaotumia soko kuhusu umuhimu wa bima ili linapotokea janga lolote wasipate hasara kubwa kama ilivyotokea kwa soko hilo Julai mwaka 2021.

Kuhusu uondoshaji wa taka, alisema soko liliweka makandarasi ambao walikuwa wanachukua taka hizo na kuzipeleka kwenye Dampo la Pugu Kinyamwezi, lakini wameanzisha utaratibu wa kuingia ubia na watu binafsi kwa ajili ya kuzirejeleza.

Mwenyekiti wa Bodi ya Soko hilo, Hawa Ghasia, alisema chanzo cha moto kwenye soko hilo kimebainika kuwa ni duka la pembejeo baada ya mwenye duka kuiacha mashine ya EFD kwenye soketi ya umeme alipokuwa anaichaji.

"Inaonyesha ile soketi ilikuwa imelegea ndipo ikashika moto wakati wa usiku na kile chumba ni cha pembejeo, walinzi wakaenda kuzima moto kwa maji wakati vile viuatilifu haviruhusu kuzimwa na maji sasa badala ya kuzima ni kama walikuwa wamekoleza moto.

"Sasa ukizingatia mpangilio wa soko wakati ule na uchakavu wa maeneo moto ukashika kasi kwa haraka, ikawa ngumu sana kuuzima".

"Moto ule umetupa fundisho tumekarabati maeneo yetu ya kupata maji, masuala ya bima yamezingatiwa na tutawapanga wafanyabiashara kisasa wasibanane ili kuwe na nafasi janga linapotokea," alisema. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Justine Lazaro, alisema kamati yake imeridhishwa na kasi ya ukarabati wa soko hilo na kuiagiza bodi ya soko hilo kuweka menejimenti bora itakayoendana na soko hilo la kimataifa.


"Tunaweza kuwa na jengo zuri, lakini kama uendeshaji usipokuwa wa kisasa tutakuwa hatujafanya lolote la maana. Kwa hiyo, wekeni mipango itakayofanya soko letu liendeshwe kimataifa na ninaamini mwenyekiti wa bodi hilo unalimudu," alisema.

Mwenyekiti alisema ugawaji wa maduka na vizimba ufanywe kwa uwazi na wafanyabiashara waliokuwapo wakati soko hilo linaungua wapewe kipaumbele ili kuepusha malalamiko.

"Jengo likamilike kwa wakati na wakandarasi wakumbushwe muda wanaotakiwa kukamilisha mradi kwasababu serikali imeshatoa fedha wao wafanye kazi usiku na mchana ili wafanyabiashara warudi waendelee na maisha yao," alisema.

Aliongeza kuwa madalali wa mazao wamekuwa changamoto kubwa kwenye masoko mbalimbali hasa Soko la Kariakoo ambapo wamekuwa wakiwanyonya wakulima wanaoleta mazao yao.

"Tuangalie namna bora ya kuwadhibiti sasa hawa madalali na kuwadhibiti kunaweza kuwa kwa njia ya kuwarasimisha ili wawe rasmi au kuwaondoa, kama tunawarasimisha basi wawe na vigezo stahiki ili mkulima anapoleta mazao yake asinyonywe," alisema.



## Teknolojia kuwakomboa wakulima vitunguu yabuniwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKULIMA wa vitunguu wanatarajia kunufaika na teknolojia ya mionzi ya kuhifadhi mazao na vyakula ili visiharibike mapema.

Akizungumza jana Jijini Arusha, wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria iliyotembelea Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) Kanda ya Kaskazini, Mkurugenzi Mkuu wa tume hiyo, Prof. Lazaro Busagala, alisema njia hiyo ya mionzi ni salama zaidi, kuliko kuhifadhi mazao kwa njia ya kemikali.

Alisema TAEC ipo kwenye mchakato wa wa uanzishwaji mradi huo, kwani vyakula vikitunzwa kwa njia ya mionzi, ni salama zaidi kuliko vile vinavyotunzwa kwa kutumia kemikali.

Alisema uhifadhi wa vitunguu kwa njia ya mionzi, unachukua miaka mitatu bila kuharibika na mradi huo unatekelezwa katika nchi 62 duniani na kwa upande wa Afrika, zipo nchi sita, ambapo Tanzania itakuwa ni nchi ya saba kutekeleza mradi huo pale utakapokamilika.

"Teknolojia hii itakapoanza itakuwa na manufaa zaidi kwa wakulima sanjari na uhifadhi wa chakula, lakini pia itakuwa mkombozi kwa wakulima na kujikwamua kiuchumi,"alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria, Florent Kyombo aliipongeza TAEC, kwa kudhibiti mionzi isilete athari kwa binadamu sanjari na vyakula.

Aidha, walimpongeza Rais Samia Hassan Suluhu kwa kutoa zaidi ya Sh. bilioni 10, kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya kisasa na kutoa fursa mbalimbali za utafiti zinazohusiana na matumizi ya nyuklia.

Alisema: "Rais Samia tunampongeza kwa kuweka ulinzi madhubuti wa kudhibiti mionzi isilete athari kwa wananchi, lakini pia TAEC inatoa huduma mbalimbali za kiutafiti katika kuhakikisha mionzi haileti athari kwa wananchi na vitu vinginevyo".

# Vijiji sita vyamwomba M/mkoa kutatua kero ya ukatili kingono

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WANANCHI wa vijiji vya Uchira, Mabungo, Koresa, Yamu Makaa, Yamu Juu na Uparo vilivyoko Kata ya Kirua Vunjo Kusini, Wilaya ya Moshi, wamemwomba Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, kutatua kero zinazowakabili ikiwamo shule mbili za msingi za Azimio na Papiliki, kutishiwa na matukio ya ukatili wa kingono.

Aidha, wananchi hao wameeleza namna wasivyoridhishwa na mwenendo wa Shule ya Sekondari Mashingia ambayo baadhi ya wazazi na walezi, wanadaiwa kuingia makubaliano ya kuandika barua ili kuwaachisha wanafunzi masomo.

Waliyasema hayo kwa nyakati tofauti wakati wa mdahalo wa jamii, uliolenga kujadili nguvu na uwezo wa wanaume kusaidia kumaliza matatizo ya ukatili wa kijinsia katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi,

Mkazi wa Kijiji cha Uchira, Jenifa Kassim, alisema yeye ni shahidi wa hilo na yuko tayari kutoa ushirikiano kwa serikali kuhusu wazazi wanaoingia makubaliano na shule hiyo ya sekondari ili kuachisha masomo watoto wao.

Mdahalo huo unaendeshwa chini ya mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust, WFT Trust (WFT-Trust).

"Kuna mtoto wa form two (kidato cha pili), ameacha shule na ni jirani yangu. Na wengineo wakiwamo wazazi wao na bibi zao, ni wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, kwa hiyo hao watoto wameshindwa kupata msaada wa kuendelea na masomo".

Salim Amir, alisema katika eneo la Uchira, matukio ya Sodoma na Gomora yanatishia ustawi wa jamii yao kutokana na baa moja (jina limehifadhiwa) kuendesha uchafu huo hadharani, hasa nyakati za mchana.

Selina Kanji, alisema ni kweli katika Shule ya Msingi Papiliki, kuna matukio ya ajabu ambayo serikali haipaswi kukaa kimya, na inapaswa kuwahoji wazazi au walezi wa watoto wanaotuhumiwa kufanya matukio ya kingono.

"Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Shule Papiliki, haya matukio tumeshayaona sana na tumeshayazungumzia sana na wazazi ndio wanaochangia kwa kweli,"alisema Kanji Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Uchira, Julius Kitero, alisema hoja ya wananchi kuhusu baa hiyo kuendesha matukio machafu ameisikia na atakutana na wajumbe wake wa Serikali ya Kijiji kulijadili na kutoa onyo, kama ikishindikana atatumia mamlaka yake kuifunga ili isiendelee kuleta madhara kwa jamii.

Alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Babu alisema: "Inawezekana vipi wewe Mwenyekiti wa Kijiji, Ofisa Mtendaji wa Kijiji na Kata, unajua matukio makubwa yanatendeka kwenye eneo lako, halafu hawaripoti kwa Mkuu wa Wilaya?"

"...kwa sababu Mkuu wa Wilaya, ndiye msaidizi wangu. Inawezekana Mkuu wa Wilaya, akawa hajui lakini kwa sababu umeniambia, niko njiani safarini, nikirudi Moshi, nitakwenda kushughulikia mimi mwenyewe."

Kabla ya mdahalo huo, Mratibu wa mradi wa jitihada za pamoja katika kuzuia na kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia, dhidi ya wanawake na watoto, Veronica Ullomi, alisema lengo la mijadala hiyo ni kujadili uwezo au nafasi ya wanaume katika kuzuia na kupambana na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.



Waandishi wa habari mkoani Arusha wakiwa katika mafunzo ya kuandika zaidi taarifa za CAG ikiwamo sheria, kuichambua ripoti na misingi ya mawasiliano baina ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Vyama vya Waandishi wa Habari. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Kina Ziwa Natroni chapungua chanzo uharibifu mazingira

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

UKANDA unaozunguka Ziwa Natron katika Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, unatishiwa na uharibifu mkubwa wa mazingira uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, serikali imekiri maji ya ziwa hilo kwa sasa yamesogea na kupungua kwa zaidi ya kilomita nne kutoka kwenye chanzo chake cha asili.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Marco Ng'umbi, kutokana na mabadiliko hayo ya tabianchi, kuathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za uhifadhi wa rasilimali asili na maliasili za ukanda huo, serikali itachukua hatua za makusudi kulihifadhi eneo hilo lisiendelee kupotea.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wenyeviti wa serikali za vijiji 39 kutoka Tarafa ya Engarenaibor, Ketumbeine na Longido, wakati Shirika la Kimataifa la World Wildlife Fund (WWF), lilipokabidhi pikipiki nne aina ya honda kwa jili ya doria, gari aina ya Toyota Landcruiser, majengo ya ofisi, kompyuta, printa na mifumo ya TEHAMA kwa jumuiya ya mpya ya uhifadhi ya LOKEEN-NATRON.

Jumuiya hiyo ya LOKEEN-NATRON, inafadhiliwa na Shirika la WWF na UK Aid.

Ziwa Natron, lina utajiri mkubwa wa ndege aina ya flamingo, ambao huzaliana kwa wingi zaidi katika eneo ambalo halina wanyama wanaowinda wanyama wengine.

Ng'umbi alisema "Kama serikali hatuwezi kukubali hilo liweze kuendelea, wenyeviti wa vijiji wa maeneo hayo mpo, kwa sababu suala la mazingira ni la kisheria, hatuwezi kulifumbia macho na hatuwezi kukubali watu wachache waharibu vyanzo vya maji, wachache waingize ng'ombe kwenye vyanzo vya maji."


Aliongeza "Julai mwishoni, nilikuwa kule Magadini, nikawa nauliza hili Ziwa Natron mwisho wake ni wapi, wakaniambia zamani hili ziwa lilikuwa linafika Shule ya Msingi Magadini, lakini leo ukiangalia kutoka pale shuleni, mpaka lilipofikia ziwa ni kama kilomita nne au tano; na linazidi kupungua zaidi. Unapoyaona haya sio bahati mbaya."

Akizungumzia athari za mabadiliko ya tabianchi, Kamanda wa Mifumo Ikolojia ya Mto wa Mbu/Longido/Lake Natron, Augustino Ngimilanga, alisema chanzo chake kinachagizwa na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea, hasa tatizo la kugombania rasilimali, kati ya binadamu, mifugo na wanyamapori.

Mifumo ya ikolijia ya Ziwa Natron, ni maarufu kwa uwindaji wa kitalii na utalii wa picha.

Msimamizi wa Mradi wa SOKNOT (Southern Kenya, Northern Tanzania) ulioko chini ya WWF, Prof. Noah Sitati, alisema kuanzishwa LOKEEN-NATRON kunawapa nguvu wananchi wa vijiji 39, kuwa na chombo chao kitakachowasaidia katika kazi za jamii.

Alisema: "Tumeanaza safari pamoja na tunapenda kuona kazi inaendelea vizuri, mliochaguliwa kuiongoza LOKEEN-NTARON, mna kazi kubwa sana na mimi bila shaka niko nyuma yenu."



# 'Speed' ya Mkurugenzi wa Halmashauri yamkosha DC

**Na Neema Sawaka,** MSALALA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, amempongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, Khamis Katimba, kwa jitihada na mikakati yake ya kimaendeleo aliyoifanya katika muda mchache tangu ateuliwe kusimamia halmashauri hiyo.

Alitoa pongezi hizo juzi wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo madiwani, wakuu wa idara na vitengo na kueleza kuwa jitihada zake zimeanza kuonekana ndani ya halmashauri katika kipindi kifupi na kuwataka viongozi wote kuendelea kumpa ushirikiano.

"Halmashauri imepata mtu makini sana, tuungane naye kuhakikisha malengo yake mapana yanafikiwa kwa muda mchache tumeona mwelekeo wake chanya," alisema.

Kadhalika alitoa pongezi kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, kwa kukubali ombi la kutoa wakufunzi wawili kuwezesha mafunzo hayo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kusimamia miradi ya maendeleo katika halmashauri hiyo.

Aidha, katika hatua nyingine madiwani hao walimuomba mkuu huyo na Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mary Mhoha, kufikisha salamu za pongezi kwa Rais Samia Suluhu Hassan juu ya utekelezaji wa miradi mbalimbali inayofanyika kwa wakati ndani ya halmashauri hiyo.

Diwani wa Kata ya Mwakata, Sixbert Ibrahim, alieleza kuwa kwa namna serikali ambavyo imekuwa ikiendelea kuongeza fedha kwa ajili ya kuimarisha sekta ya elimu, afya, barabara, maji na nishati ya umeme vijijini kupitia REA hali inayoongeza kasi ya maendeleo ya halmashauri.

Aidha, mafunzo hayo pamoja na mambo mengine yalilenga viongozi hao kujua mipango ya bajeti ya halmashauri inayopanga, hivyo kuwa rahisi kwao kufanya ufuatiliaji katika ngazi mbalimbali na kuhakikisha usimimizi wake unafanyika kwa ufanisi na kudhibiti mianya ya wizi wa fedha za umma.

Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Mohamed Mbega aliwataka viongozi hao kufanya kazi kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni ili kulinda heshima na maadili ya uongozi.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Abdallah Urari, aliwaomba viongozi hao kutoa ushirikiano kwa maofisa wa taasisi hiyo.

Alisema taarifa za udanganyifu katika ukusanyaji mapato na matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa baadhi ya wataalamu na viongozi wa halmashauri hiyo pamoja na ufisadi kwa madiwani zipo mezani kwake.



Mwezeshaji wa Masuala ya Jinsia na Afya ya Uzazi, Fortunata Scander, akitoa mada katika semina ya elimu ya uzazi kwa baadhi ya wafanyakazi wa ndani pamoja na viongozi wa mitandao ya wafanyakazi wa ndani kutoka mikoa sita nchini, yenye lengo la kuwawezesha kujilinda na kuwalinda watoto wa waajiri wao dhidi ya mabadiliko mbalimbali ya kiafya katika kipindi cha balehe. Mafunzo hayo yanasimamiwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Wote Sawa. **PICHA: VITUS AUDAX**

## DC Nyamagana atoa maagizo matatu kwa MWAUWASA

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mwanza (MWAUWASA) imekumbushwa kufanya usimamizi makini katika miradi tegemewa ya maji kuhakikisha inakamilika kwa wakati, mojawapo ni mradi wa usambazaji maji Butimba.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, baada ya ukaguzi wa mradi huo unaotekelezwa kwa usimamizi wa MWAUWASA ambao mpaka sasa umefikia asilimia 94 ya utekelezaji wake.

Alisema hatua ambayo mradi umefikia ni kubwa, kuwakumbusha wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha wanaongeza juhudi katika kusimamia na kuhakikisha mkandarasi anatekeleza majukumu yake ipasavyo kuondoa adha kwa wananchi.

"Kwa sasa kazi inaenda vizuri na kwa kipindi kifupi tumeona mabadiliko makubwa katika utekelezaji na kwa kasi hii tunapata matumaini kwamba utekelezaji utakamilika ndani ya muda na huduma itapatikana kama ilivyokusudiwa," alisema Makilagi

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Neli Msuya aliahidi kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi yote iliyopo chini ya mamlaka hiyo lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa wakati.

Alisema kuwa kazi za ujenzi katika mradi huo zipo katika hatua za mwisho na mkandarasi anafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha wanakamilisha kila hatua kwa muda uliopangwa na majaribio yatafanyika Septemba 15 mwaka huu.

Mradi wa Maji Butimba unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya serikali, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa kwa gharama ya Sh.bilioni 69.

Mradi huo utakapokamilika utaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa wakazi wapatao 450,000 waishio maeneo ya pembezoni.

# Madiwani waweka ngumu ukodishwaji mitambo barabara

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wamekubaliana kutoendelea kukodishwa kwa mitambo ya kutengeneza barabara iliyonunuliwa kwa fedha ya mapato ya ndani kwa makandarasi binafsi.

Pia, wamemuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Hadija Kabojela, kuhakikisha mitambo hiyo inafanyakazi iliyokusudiwa ya kufungua mtandao wa barabara zao za vijijini.

Mitambo hiyo ni motor grader, compactors roller, low bed, tractor hea pamoja na excavator iliyonunuliwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 1.4, lengo likiwa ni kufungua mtandao wa barabara vijijini na badala yake iliishia kukodishwa kama sehemu ya chanzo cha mapato ya ndani.

Maazimio hayo yalifikiwa hivi karibuni katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2022/2023 kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya elimu, afya, maji, kilimo na barabara.

Pamoja na mambo mengine madiwani hao waliiagiza ofisi ya mkurugenzi kununua ving'amuzi na kufungwa katika mitambo hiyo.

Diwani wa Kanamapula, Sharifu Samweli, alisema mwaka wa fedha 2014/2015 walikubaliana kununua mitambo hiyo kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kwa lengo la kufungua mtandao wa barabara vijijini ili kurahisisha usafirishaji wa mazao hadi sokoni, lakini iliishia kukodishwa baada ya kununuliwa.

Alisema kama isingekuwa inakodishwa kwa makandarasi mbalimbali ingekuwa imeshafungua na kukarabati barabara nyingi kwa sababu mwaka wa fedha 2019/2020, akitolea mfano wa aliyekuwa Mbunge wa Ushetu Eliasi Kwandikwa alitoa lita 433.44 za mafuta kupitia fedha za mfuko wa jimbo ili mitambo ifanyekazi lakini mpaka sasa hayajatumika.

Michael Bundala, Diwani wa Kisuke alisema kuwa hivi karibuni Mbunge Emmanuel Cherehani ametoa Sh. milioni nane za mfuko wa jimbo kwa ajili ya mafuta na kuwalipa waendesha mitambo na kufungua barabara katika Kata ya Kinamapula, Kisuke na Ubagwe lakini mitambo ilikuwa imekodishwa.

Diwani Robert Mihayo alisema: "Halmashauri hii inategemea mapato kutoka kwenye kilimo kwa asilimia kubwa, barabara zetu ni mbovu zinahitaji matengenezo ili mazao yafike sokoni kiurahisi na tupate mapato, mitambo tunayo ila tunashindwa kuitumia kwa sababu tumeikodisha".

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Hadija Kabojela, aliahidi kuisimamia mitambo hiyo na kuhakikisha inafanyakazi iliyokusudiwa kwa kushirikiana na kamati ya usimamizi iliyochaguliwa.

Alisema hivi karibuni imeokoa Sh. milioni 111 iliyotakiwa kutumika katika kufungua barabara endapo ingekuwa imekodiwa.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri, Gagi Lala alisema muda mrefu mitambo hiyo walikuwa wakiikodisha kwa makandarasi kama sehemu ya chanzo cha mapato ya ndani, lakini fedha zilizokuwa zikipatikana ziliishia kwenye matengenezo na wao kukosa fedha hali iliyowafanya kuendelea kuikodisha.



Ukurasa 12

Mikakati kiubunifu itakavyo wakwamua vijana kubeti, kupoteza muda na umakini





Ukurasa 14

Japan inavyojikuta njia panda majasusi wakiibia teknolojia, ubunifu kiurahisi

Nipashe

TESA

Jumanne Agosti 29, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 13

AMDT, ADDA tumaini jipya kinamama kutoka umaskini hadi wamiliki viwanda

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Ni kizaazaa wasichana hawa wanapojisaidia vichakani

TATIZO la ukosefu wa vyoo shuleni ni jambo linalowaathiri zaidi mabinti ikilinganishwa na wanafunzi wa kiume. Ni vigumu kwa wanafunzi wa kike kujisaidia vichakani, lakini pia huvurugikiwa zaidi wakati wa siku zao kwa sababu hakuna sehemu ya kujisitiri wala kutupa taulo zilizozotumiwa.

Shule ya Msingi Kiloleli iliyoko Kishapu mkoani Shinyanga, haina vyoo na kama ilivyo ada wanaoathirika zaidi ni wasichana ambao wanakosa chumba cha kujistiri lakini pia wanaona aibu kujisaidia vichakani ili kulinda utu na heshima.

Wanahofia kwenda haja vichakani kutokana na uwezekano wa kunyanyaswa na kukejeliwa na hata kuumizwa ikiwamo kurushiwa mawe na watu wasiowafahamu.

Shuleni hapo vyoo ni vibovu na havifai tena kwa matumizi, anasema Mwalimu Mkuu Msaidizi Juliana Petro, akiongeza kuwa idadi ya wanafunzi ni 997, ambao wote wanajisaidia vichakani.

Aidha, anasema vyoo vya shule hiyo ni vibovu na havifai kutumiwa kwa sababu vinahatarisha usalama wa wanafunzi na afya zao, hivyo wakalazimika kuwazuia wasiendelee kuvitumia, bali watumie njia nyingine ikiwamo kwenda vichakani.

"Ni hatari kiafya shule kutokuwa na vyoo, na hapa hatuna hata maji ila tunashukuru wananchi wa Kiloleli wamehamasika na kuanza kujenga matundu 24 ya vyoo," anaongeza Mwalimu Juliana.



Choo kibovu katika Shule ya Msingi Kiloleli. **PICHA: MARCO MADUHU**

Mwanafunzi Mary Joseph, anazungumzia hali hiyo akisema ukosefu wa vyoo unawapa shida nyingi wasichana. Mosi wanakosa eneo la kujisaidia lakini ugumu unajitokeza zaidi wakati wa siku zao, yote hayo yakiwasababishia wakati mwingine kuchukia kwenda shule hali inayoongeza utoro na hata kuwa na idadi kubwa ya wasichana wasiohitimu elimu ya msingi.

"Wanafunzi wa kike siyo kama wa kiume, sisi tunahitaji usiri mkubwa, sasa kwenda kujisaidia vichakani siyo jambo jepesi tena si maadili na ukimaliza kujisaidia hakuna hata maji kwa ajili ya usafi, wakati mwingine tunarudi nyumbani kujisaidia hasa wanaoishi jirani. Lakini wapo wenzetu wengine huondoka moja kwa moja bila kujali kinachoendelea darasani,"anasema Mary.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiloleli Kuhwema Mshala, anasema changamoto hiyo ya ukosefu wa vyoo Kiloleli wanaifahamu, na wameanza kuchukua hatua. Hivi karibuni walikutana na wajumbe wa kituo cha taarifa na maarifa kinachojengewa uwezo na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP)kuibua matatizo ndani ya jamii, na sasa wanatafuta namna bora ya kushirikiana kuitatua.

Anasema waliitisha mkutano wa hadhara wa kijiji na wakakubaliana kila kaya kuchanga Shilingi 2,000 pamoja na kujitolea nguvu kazi ili kusomba mchanga, mawe, kokoto na kuchimba shimo la choo.

Anasema serikali ya kijiji kupitia mfuko wake nayo ilitoa Shilingi 600,000 na Jeshi la Jadi Sungusungu Shilingi 500,000 na kuanza ujenzi wa matundu 24 shuleni hapo.

Mtendaji wa Kijiji cha Kiloleli, Nicholaus Mzirai, anasema katika mchango wa fedha wananchi wamechangia Shilingi 700,000 na kwamba katika pesa walizopata za ushuru wa pamba Shilingi milioni 1.3 walikubaliana kutenga Shilingi 500,000 na kuzielekeza kwenye ujenzi wa vyoo shuleni hapo.

"Serikali ya kijiji tunashukuru wananchi kuhamasika na kuchangia shughuli za maendeleo, kwa sababu watoto wanaosoma katika shule hii ni wetu hivyo ni vyema kuwawekea mazingira mazuri ya kusoma kwa kuwajengea vyoo na kulinda usalama na afya zao,"anasema Mzirai.

Mkazi wa kijiji cha Kiloleli, Martha Ngwelu, anasema baada ya kuhamasishwa kujenga vyoo katika shule hiyo, waliitikia kutokana na hali ambayo walijionea wazazi na walezi jinsi kulivyokuwa na kuhatarisha afya za watoto wao.

Mjumbe wa kituo cha taarifa na maarifa kutoka Kiloleli, Helena Makelele, anasema baada ya kufika katika shule hiyo na kujionea vyoo vilivyokuwa katika hali mbaya na kufungwa, tena na kupokea taarifa za wanafunzi kuwa wanajisaidia vichakani, wakaanza kupanga mikakati na kuchukua hatua.

Anasema hatua mojawapo ni kushirikiana na uongozi wa kijiji na kukubaliana kuhamasisha wananchi kuchangia ujenzi wa vyoo na siku ya mkutano wakafanya harambee na kupatikana Shilingi 50,000 na mifuko mitano ya sementi.

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA DK FELICIAN KILAHAMA

# Mikakati kiubunifu itakavyowakwamua vijana kubeti, kupoteza muda na umakini

***MAKALA hii ni mwendelezo wa masuala ya vijana ambayo ilichapishwa wiki iliyopita, ilimalizika kwa kuwataja vijana kuwa wanapenda wakati mwingine kupata fedha kirahisi mfano, kupitia masuala ya 'ku-beti'. Ikiwa hili ndilo 'jembe la taifa' nguvu kazi na ndiyo wanaotazamiwa kuibeba nchi, wanahitaji jicho la ziada, kuwafikisha kwenye ujana wenye tija.***

Eneo mojawapo linalohitaji kutupiwa macho ni nguvu kazi hii kuiepusha na kujiingiza kwenye kubeti na michezo mingine mingi inayochezwa kupitia mitandao na vyombo mbalimbali vinavyohimiza Watanzania kucheza ili kujipatia fedha kirahisi.

Haya yote yanafanyika kwa mwelekeo wa kamari na vijana wengi wamevutwa. Kimsingi masuala yanayohusiana na kucheza kamari siyo mazuri maana yanapelekea wahusika kupotoka na kujikuta kwenye uhalifu.

Kwanza, kuna kutekwa kifkra au kiakili na kupoteza maarifa ya kufanya maamuzi sahihi, kila wakati mhusika anabaki akijiweka kwenye nafasi ya kushinda tu, huku akitumia fedha ambazo harudishiwi iwapo hatashinda.

Pili, michezo ya aina hiyo, inajenga 'lango' la kutenda uhalifu ikiwamo wizi na udanganyifu, iwapo kijana hana fedha za kucheza, atafanya kila linalowezekana apate pesa kihalali au vinginevyo ili mradi afanikishe lengo.

Kihalali anaweza kuuza vitu vyake mfano, nguo, viatu, simu au akahangaika akapata kibarua na kupata fedha akacheze kwa mtazamo kuwa atashinda na kupata fedha atajirike haraka.

Vinginevyo, kuna uwezekano mkubwa kujenga tabia ya kudokoa mali za wengine au kuiba fedha na vitu vingine nyumbani, mitaani na hata kupora ili mradi afanikishe lengo lake.

Kwa bahati mtazamo huo usiofaa kwa vijana ambao ndiyo nguvu kazi kubwa ya taifa letu, unachochewa na baadhi ya matangazo yanayofanyika kupitia vyombo mbalimbali mathalani, runinga, radio, magazeti na hata simu janja au viswaswadu.

Kuna wakati unapofungua ujumbe kwenye simu; mara kwa mara kuna ujumbe fulani zinazotangaza kuwa 'wewe umekaribia kushinda kiasi fulani cha fedha mathalani, milioni 10, tuma 'neno hili' ushinde.

Ukiangalia tarakimu hizo na



Vijana wasio na la kufanya wakikaa vijiweni mitaani kusubiri jua lizame. **PICHA: MTANDAO**

> Michezo inawafanya wengi wapoteze fedha zao kwa matumaini ya kupata au kushinda bila kujua wanaoshinda ni wachache sana kulingana na idadi ya wanaocheza.

kwa lugha ya mitaani kwa 'buku' tu anahamasika kucheza, lakini ili aweze kushinda na kupata hizo fedha atacheza mara ngapi? Yote haya ni katika kugeuza akili za wengi na hasa vijana ambao ndiyo kundi kubwa linaloathirika zaidi.

Wakati mwingine yanaletwa maswali kadha wa kadha na mengi ni ya kimichezo hasa soka au kuigiza pia nyimbo hasa 'bongo fleva' na waimbaji wake. Nia ni watu wengi wajibu ili kuongeza mapato

Michezo inawafanya wengi wapoteze fedha zao kwa matumaini ya kupata au kushinda bila kujua wanaoshinda ni wachache sana kulingana na idadi ya wanaocheza.

Kabla mhusika hajacheza mchezo wowote wa kubahatisha, ni lazima kujua asilimia ya ushindi au uwezekano wa kushinda (probability rating) na hilo ni jambo la msingi. Kwa mfano, kuna wachezaji 1,000,000 kwa mchezo mmoja na pengine anatakiwa apatikane mshindi mmoja, washindi 10 au 100. Kinachotakiwa kukifahamu ni kujua kwa kiasi gani unaweza kushinda?

Kwa kundi la kwanza zitatolewa 1,000,000 pili milioni 10 na la tatu milioni 100, kiwango cha ushindi ni asilimia 0.0001, 001 na 0.01 kwa makundi hayo matatu sawia, hali hiyo inaonyesha kuwa ni asilimia ndogo sana ya mhusika kuweza kuibuka mshindi ndiyo maana ikaitwa 'Bahati nasibu'.

Kadhalika, baadhi ya vijana hutembeza barabarani bidhaa mbalimbali mikononi wakitafuta wateja. Wengine wanatumia muda mrefu kutoka eneo moja kwenda jingine wakitafuta wanunuzi.

Jioni wanapoona hawana kitu mfukoni na njaa 'imekaza uzi' wanalazimika wauze kwa bei mnunuzi anayotaka ili mradi apate kiasi cha kumsaidia kujikimu.

Baadhi wanafamilia hivyo kujikuta katika changamoto hatarishi kiasi cha kulazimika kutenda uhalifu kwa kigezo cha 'hakuna jinsi' bora nusu shari kuliko shari kamili anaitelekeza familia yake.

Tujiulize kwa mstkabali wa taifa letu je, vijana kutaka kupata fedha haraka haraka kupitia michezo mbalimbali ya kifedha kama kubeti kitaifa ni jambo jema? Je, vijana na watu wengine tunatumia muda vizuri kwa manufaa yetu, familia na taifa pia?

Kimsingi, matumizi halisi ya muda kwa nyakati hizi ni suala la kuwekewa mkazo. Kila siku tunapoamka tunafanya nini? Maana unakuta makundi ya watu, rika mbalimbali, wakiongelea masuala ya michezo, mfano, kusajili wachezaji, hususani timu za Tanzania na Ulaya.

Kadhalika, unaona vijana wanatumia muda mwingi kwenye mitandao ya kijamii 'wakichati' kupitia simu janja. Je, ni matumizi halisi ya muda? Siku ina saa 24, na wiki siku saba ina saa 168. Kawaida binadamu anatakiwa kulala usingizi (angalau saa nane kwa siku, kwa wiki atatumia saa56 usingizini).

Wiki ukiondoa siku moja ya kuabudu au kusali kuna siku sita za kufanyakazi. Hii ina maanisha kuwa tukiondoa saa za kusinzia; kwa siku tuna saa 16 za kufanyakazi na ndani ya siku sita ni takribani saa 96 za kufanyakazi.

Muda huu ukitumiwa kwa kiwango cha kufikia asilimia 75 takribani saa 12 kwa siku sawa na saa 72 kwa wiki, ukatumika kuzalisha mali na huduma ili kujipatia kipato, hakika nchi itajikwamua kimaendeleo na muda uliobaki takribani saa 4 kwa siku au saa 24 kwa siku sita za kazi; ukatumika kwenda na kutoka mahali pa kazi, pengine kupata mapumziko mafupi wakati mhusika akiwa kazini.

Uzoefu unaonyesha kuwa wengi wetu, wakiwamo vijana, hatuzingatii matumizi mazuri ya muda iwe ofisini, viwandani, nyumbani au kwingineko; bado kuna kusuasua bila maelezo ya kutosheleza. Vijana wajiepushe na kufuata mkumbo kwa masuala yasiyotuletea maendeleo ya kweli kimaisha.

Serikali iweke sera thabiti kuinua maisha ya Watanzania hususani vijana. Tuliporuhusu matumizi ya bodaboda na bajaji kutoa huduma za usafiri na usafirishaji; jambo hilo limekuwa faraja kwa vijana wengi kujiajiri au kuajiriwa. Wanaoitumia fursa hiyo kwa umakini, baada ya miaka michache wanasonga mbele.

Mkakati wa serikali wa kuinua zaidi shughuli za kilimo kwa lengo la kuwapatia vijana ajira na kuimarisha au kuendeleza uchumi wa taifa; upewe msukumo zaidi ili kuhusisha sekta mbalimbali za umma na binafsi

Kupanuliwe wigo ili vijana wengi waweze kujipanga kikamilifu kulingana na uwezo wao, wenye ari ya kufuga wafanye hivyo, kitaaluma au kibiashara, wenye kumudu masuala ya uvuvi, misitu, nyuki na utalii pamoja na biashara wafanye hivyo pia.

Kadhalika, shughuli za ugani ziimarishwe kuhakikisha mafanikio yanayotarajiwa yanapatikana. Tukiongeza tija na bidhaa nyingi kuzalishwa hapa nchini; tutajenga uwezo wetu kujitegemea. Wakati huo huo, tutasaidia idadi kubwa ya vijana kuachana na michezo isiyowasaidia, hivyo kuimarisha nguvu kazi ya taifa letu kwa faida ya wengi.

Halmashauri nchini na mamlaka za mikoa na wilaya; zihakikishe kuna mazingira bora ya kuwezesha vijana kutumia ardhi kwa faida na weledi mathalani, zianzishe mifumo thabiti ya kuunganisha vijana kwenye maeneo yao.

ELIMU

NA MAULID MMBAGA

# AMDT, ADDA tumaini jipya kinamama kutoka umaskini hadi wamiliki viwanda

## • Mbioni kumaliza uhaba, ulanguzi mafuta ya kula



Braunes Chengula, mwekezaji wa kilimo cha alizeti na uzalishaji mafuta akiwa kiwandani kwake Wanging'ombe mkoa wa Njombe. **PICHA: MAULID MMBAGA**

MAFUNZO ya kilimo bora, kutumia teknolojia, mbegu na uwepo wa masoko kwa wanawake katika mikoa mbalimbali kumewawezesha kutembea kifua mbele baada ya kuwekeza kikamilifu mashambani.

Wakijikita kwenye matumizi ya mbegu bora za alizeti na kilimo cha kisasa juhudi hizo zimewawezesha kupata mazao zaidi na kukua kibiashara na sasa wanamiliki viwanda.

Matumizi ya teknolojia ya kisasa, pembejeo na mbegu bora vimeongeza uzalishaji mavuno kwa wingi, kusindika alizeti kisasa na kupata mafuta yenye ubora na sasa wengine wanamiliki viwanda.

Mafanikio hayo ni ya mradi wa taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT), wenye lengo la kutoa elimu, kuhamasisha matumizi ya teknolojia, mbegu bora za alizeti na kilimo cha kitaalamu.

Baadhi ya shuhuda zinatoka kwa kinamama wanufaika ni kama hizi: Eva Tomson mkulima anayemiliki kiwanda cha kuchakata alizeti kilichopo Kibaigwa Dodoma, anasema alianza uwekezaji 2017, wakati huo biashara haikuwa na tija sababu uelewa mdogo na miundombinu duni ya kilimo.

Alikuwa na mashine moja lakini baada ya kuwezeshwa kitaalamu na taasisi ya Maendeleo ya Kilimo Denmark Asia (ADDA) Tanzania inayoshirikiana na AMDT anainuka baada ya kupata mashine iliyoongeza uchakataji na kupata madumu 200 ya mafuta kwa siku badala ya 50 hapo zamani.

Hadija Iddi, anaishi Kibaigwa pia, ana kiwanda cha kuchakata alizeti. Anajivunia mafunzo aliyoyapata ADDA chini ya mradi wa AMDT na sasa ameongeza soko na mapato. Anasema awali walikuwa wanatumia madalali kununua alizeti leo wanakutana na wakulima moja kwa moja jambo linalowapunguzia gharama za manunuzi.

"Mafunzo ya AMDT yametukutanisha wafanyabiashara na wakulima, awali ugumu ulikuwepo hasa kwenye suala la soko wakati wa kununua mbegu unajikuta uko katikati ya madalali na wakulima, mnunuzi unapigwa hela kotekote ilimradi upate mbegu lakini kwa sasa hali hiyo haipo," anasema Hadija.

Hawa Abdial, mwenye kiwanda cha kuchakata alizeti Dodoma, amenufaika pia na ADDA Tanzania na AMDT, akipata mashine ya kisasa na kuwezeshwa kutengenezewa miundombinu ya kisasa ya kusafisha mafuta na kuongeza ubora wa bidhaa anazozalisha.

"Mwanzoni nilikuwa nabahatisha, sasa naweza kuzalisha zaidi ya kilo 300,000 kwa kipindi chote cha msimu, tofauti na awali nikishia kilo 180,000. Hiyo kwangu ni hatua kubwa kunijengea uaminifu kwa wateja wangu, walioongezeka kutokana na kuongezeka ufanisi na ubora."

"Nawashukuru walionipa mafunzo kuanzia, SIDO na AMDT, nilikuwa sina cha kufanya, nilienda nikawaambia nina mashine lakini sina njia ya kutokea na walinishika mkono na kunisaidia kufanikisha uchakataji," amesema Hawa.

Zuhura Mpinga, mkazi wa Kijiji cha Mayale mkoani Njombe, anasema alianza biashara ya mafuta miaka 10 iliyopita akiwa na mashine moja ya kukamua licha ya kwamba hakuwa na uelewa kuhusu kuchakata.

Anasema baada ya siku chache alikutana na taasisi iliyomshauri na kumkosoa kutokana na mfumo aliokuwa akiutumia na kumshauri kujiendeleza kitaalamu. "Nilifuata mafunzo waliyonipatia pia walinipeleka Dodoma kwa mafunzo, pia nilifundishwa namna ya kuweka kilimo mkataba na sasa wamenipokea watu wa AMDT," anasema Zuhura.

### UWEKEZAJI MKUBWA

AMDT imewekeza zaidi ya Shilingi bilioni nne kwa ajili ya kuongeza mnyororo wa thamani na tija katika kilimo nchini, kwa wanawake wanaosindika alizeti, ikiwasaidia mafunzo, vifaa vya kisasa na teknolojia kuwawezesha kuendesha shughuli za kukamua na kuzalisha mafuta bora ya alizeti inayolimwa kwa ubora.

Meneja wa mradi unaohamasisha kilimo chenye tija kwa upande wa ADDA Tanzania, Mercy Kingo, anasema wanashirikiana na wakulima na wasindikaji wadogo wa alizeti wanaofadhiliwa na AMDT ili kuongeza mnyororo wa thamani na kufikia uwekezaji wenye tija. Anajivunia mafanikio kwa kina mama wanaosindika alizeti ambao ni miongoni mwa washirika wao, na kwamba wamewawezesha pia kuwa na vigezo vya kukopa kwenye taasisi kubwa za kifedha pamoja na kuingia mikataba ya manunuzi na wakulima wadogo.

Mercy anakiri kinamama wengi walikuwa na upungufu mfano kukosa mitaji na uwezo wa kusimamia na kuendesha viwanda vidogo na kwamba AMDT na ADDA Tanzania wakiwa miongoni mwa washirika katika utekelezaji wa mradi wamefanya jitihada mbalimbali kuwainua wajasiriamali hao na kukuza biashara zao.

"Pia tumewawezesha kutunza taarifa zao, waone faida ya kinachoingia na kutoka katika biashara wanayoifanya, pamoja na kuhakikisha viwanda na mitambo wanayoitumia kusindika inakuwa ya kisasa ili watoe mafuta yenye ubora," anasema Mercy.

> Tunafanya kazi pia na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) na katika utekelezaji tunataka wasindikaji wadogo wafanye kazi na wakulima wadogo ili kuongeza mnyororo wa thamani wa alizeti.

"Katika kufanikisha hilo mradi unatoa asilimia 60 katika kununua mashine za kisasa na wenyewe wanatoa asilimia 40 ya fedha, lakini pia tunawasaidia bidhaa wanazozizalisha zinapata masoko na waweze kufahamika."

Anaeleza kuwa wanawasaidia pia kupata vibali vya Shirika la Viwango (TBS) pamoja na kuhakikisha miundombinu ya mahali wanapofanyia kazi inakidhi viwango.

Anasema wamewaelimisha pia namna ya kutunza faida zao, kurekebisha mazingira ya viwanda, kufanya kazi kwa utaratibu maalumu, na kuboresha miundombinu jambo ambalo limesaidia kuongezeka kwa ubora wa mafuta na kuwavutia wanunuzi wengi.

Anabainisha kuwa wanafanya kazi pia na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) ili kuhakikisha viwango vya viwanda wanavyoviendesha kina mama hao vinakua sawa, na kwamba washirikiana pia na shirika la Brazil linalotoa huduma za kijamii viwandani (SESI) kuwapa mafunzo.

"Tunafanya kazi pia na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) na katika utekelezaji tunataka wasindikaji wadogo wafanye kazi na wakulima wadogo ili kuongeza mnyororo wa thamani wa alizeti," anasema Mercy.

### MALENGO AMDT

Mtendaji Mkuu wa AMDT, Charles Ogutu, anasema uwekezaji unalenga kuiwezesha miradi inayoendeleza alizeti na mikunde, kusaidia vipaumbele vya serikali katika kilimo na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDPII)

Pia inaelezwa kuwa mfuko wa maendeleo ya masoko ya kilimo AMDT unafanya kazi ili mapato na fursa za ajira za wanawake maskini, wanaume na vijana ziongezwe katika minyororo ya thamani ya kilimo.

Aidha, anasema taasisi inalenga kufikia azma hiyo kupitia matokeo mawili, la kwanza ni wakulima na wajasiriamali wadogo wanaweza kushindana na kufanikiwa zaidi katika masoko ya kilimo yaliyochaguliwa na kwamba kazi zinazowasaidia zinaboreshwa.

Ya pili ni kuweka mazingira wezeshi, kuboreshwa katika minyororo ya thamani ya kilimo ikiwemo sheria, kanuni, sera, taarifa, maarifa, uratibu na uaminifu, anaongeza Ogutu.

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

# Japan inavyojikuta njia panda majasusi wakiibia teknolojia, ubunifu kiurahisi

KESI ya madai ya kuvuja kwa teknolojia inayomhusisha mtafiti wa China katika taasisi ya juu ya utafiti ya Japan inachukuliwa kama mwanzo wa kuanza kufanya mambo kwa tahadhari zaidi, kulinda usalama wa taifa,

Ni baada ya Quan Hengdao, mtafiti mkuu mwandamizi katika Taasisi ya Kitaifa ya Sayansi ya Juu ya Viwanda na Teknolojia (AIST), mjini Tsukuba, katika mkoa wa Ibaraki nchini Japani, hivi karibuni alikamatwa kwa tuhuma za kutoa siri za kiteknolojia.

Anadaiwa kuvujisha data iliyopatikana kama sehemu ya kazi yake katika AIST kwa kampuni ya China, kinyume na sheria inayokataza ushindani usio wa haki.

Quan (59) amefanya kazi Japan tangu Aprili 2002 lakini pia akawa profesa katika Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Beijing mwaka 2006, kulingana na uchunguzi wa gazeti la Sankei.

Chuo Kikuu cha Beijing na kile cha Sayansi na Teknolojia cha Nanjing ambapo alikuwa mwanafunzi, ni taasisi muhimu katika "Wana Saba wa Ulinzi wa Kitaifa," ikimaanisha kuwa zina uhusiano na Jeshi la China.

Aidha, Quan alikuwa sehemu ya programu ya "Thousand Talents" ya serikali ya China, ambayo inalenga kuvutia watafiti katika nyadhifa muhimu kuendeleza uwezo wa Beijing wa kisayansi na kiteknolojia.




**TUHUMA ZAKE**

Quan anashutumiwa kutoa data za siri za teknolojia za kuunganisha misimbo ya florin (florine codes) kwa mradi wa biashara nchini China ambao alianzisha na mkewe.

Miezi michache baada ya data hizo kutumwa, kampuni ya wanandoa hao ilipata hati miliki ya teknolojia hiyo nchini China.

Taarifa ambazo Quan alitoa "hazionekani kuwa zinazohusiana na ulinzi au teknolojia zinazohusiana na usalama wa kiuchumi," anasema Jin Matsubara, Mwenyekiti wa zamani wa Tume ya Kitaifa ya Usalama wa Umma ambaye kwa sasa ni mwanachama wa Chama cha Kidemokrasia cha Kikatiba cha Japan, chama cha siasa za mrengo wa kushoto ambacho ni kikubwa zaidi cha upinzani bunge la Japan.

Lakini kesi hiyo inaangazia uharibifu unaoweza kusababishwa kwa Japan, anasema, na kuongeza kuwa "Inapaswa kuwa kama kelele inayoamsha tahadhari kwa serikali".

"Ni muhimu kutathmini kesi hii kwa mtazamo mpana," anasema. "Kuna malengo mawili ya sheria za Japan kuhusu sayansi na teknolojia; la kwanza ni kuzuia kupotea kwa teknolojia za hali ya juu na la pili ni kukuza mabadilishano ya kimataifa na kuwaalika watafiti wa kigeni wenye ujuzi na vipaji vya kipekee ili kushirikiana na wataalam wa Japan," Matsubara anaongeza.

"Ndio maana kuna Wachina na Warusi wengi katika taasisi za utafiti na vyuo vikuu nchini Japan," anaiambia DW.

"Watafiti hao wa kigeni wamekuwa muhimu sana kiasi kwamba taasisi zingine haziwezi kufanya kazi bila wao."

China na Marekani ziko kwenye vita vya kibiashara, ambavyo ni vikwazo vya kushiriki teknolojia ya kisasa.

Japani na mataifa ya magharibi kama Marekani zimezidi kuwa na wasiwasi katika miaka ya hivi karibuni kuhusu uhamisho wa teknolojia ya kisasa kwenda China.

Utawala wa Rais wa Marekani Joe Biden, unasema unataka kuzuia teknolojia ya hali ya juu ya nchi za magharibi kununuliwa na vikosi vya Jeshi la China na mashirika ya kijasusi. Mwaka jana, Washington iliweka vizuizi kwa China kupata 'chip' za kisasa na vifaa vya kutengeneza chip, sababu ikielezwa kuwa ni usalama wa taifa.

Japan na Uholanzi pia hivi karibuni zilitangaza vikwazo vipya vya usafirishaji wa bidhaa kwenye teknolojia ya utengenezaji wa chip, bila kuitaja China.

**UPO UTETEZI**

Matsubara anadokeza kwamba masharti ya sheria ya kitaifa ya ujasusi ya China yanawataka Wachina wote kutoa maarifa yote waliyopata ng'ambo kwa serikali, licha ya makubaliano yoyote ya kutunza siri ambayo wanaweza kuwa wametia saini kwenye mataifa ya kigeni.

Na hiyo ina maana kwamba "Kila Mchina ana uwezo wa kuwa jasusi, anaiambia" DW.

"Hii ndiyo sababu nchi kama Japan na Marekani hazina chaguo bali kuwatenga watafiti wa China kutoka taasisi zinazoshughulikia teknolojia nyeti sana za kiuchumi au zinazohusiana na usalama kupitia utumiaji mzuri wa mfumo wa kibali cha usalama," anasema.

**MAJASUSI WENGI**

Swali hili linaulizwa kuna majasusi wengi zaidi nchini Japan? Na jibu linakuwa wengine wanaamini kwamba awamu za serikali za Japan zilizofuatana zimeshindwa kuchukua tahadhari zinazohitajika na kwamba usalama wa taifa hilo unahatarishwa.

"Sielewi jinsi Quan alivyoruhusiwa kubaki katika wadhifa huo kwa miaka 20 bila kuchunguzwa," anasema Yoichi Shimada, Profesa wa Uhusiano wa Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Jimbo la Fukui.

"Kwangu hii inaonyesha tu jinsi tulivyolegea linapokuja suala la mustakabali wa kiuchumi wa Japan na usalama wetu wa siku zijazo. Kwa kweli ni jambo lisilosameheka."

Shimada anasisitiza kuwa ana hakika kuna majasusi wengi zaidi kutoka China na kwingineko nchini Japan. Anatoa wito kwa serikali kutosubiri tena ianze kushughulikia tatizo hilo.

"Hisia yangu ni kwamba serikali hii na vyuo vikuu wamekuwa dhaifu sana juu ya matatizo haya na hii imedhihirisha ukubwa wa kadhia," anaongeza.

## Ni kizaazaa wasichana hawa wanapojisaidia vichakani

INATOKA UK.11

Anasema katika ujenzi wa matundu hayo 24 ya vyoo shuleni hapo, kutakuwapo pia na chumba maalumu kwa ajili ya wanafunzi wa kike kujistiri na kueleza kwamba ujenzi umefikia hatua ya kufunga lenta na kuwashukuru wananchi kujitoa ili kulinda afya za wanafunzi na wananchi majirani na eneo hilo.

Diwani wa Kiloleli, Edward Manyama, anasema tatizo la ubovu wa vyoo katika shule hiyo analifahamu, na wamekuwa wakizungumza kwenye vikao vya kata kuona namna ya kulitatua, na kushukuru wananchi wameanza kulifanyika kazi.

Ofisa Elimu wa Shule za Msingi na Awali Halmashauri ya Kishapu, Angasirini Kweka, anasema ujenzi wa matundu ya vyoo katika Shule ya Kiloleli umetengewa Shilingi milioni 13 na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kishapu imechangia Shilingi 600,000 ili kuunga mkono nguvu kazi za wananchi katika ujenzi wa vyoo.

Anasema halmashauri hiyo ina upungufu wa matundu ya vyoo 2,626 kwa shule za msingi na kwamba yaliyopo ni 1,281 huku mahitaji ni 3,907 na katika mwaka wa fedha 2023/2024, ulioanzwa kutekelezwa mwezi uliopita Julai mosi, Shilingi milioni 126.4 zimetengwa kwa ajili ya kujenga matundu 114.

Aidha, anasema kuwa katika mpango shirikishi wananchi wanatarajia kujenga matundu 1,004.





## Magereza yaanika mikakati kupunguza msongamano wafungwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMISHNA Jenerali wa Jeshi la Magereza, Ramadhan Nyamka, amesema wafungwa 29,012 wapo kwenye magereza mbalimbali nchini, huku akianika mikakati ya kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za jeshi hilo ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wake, Nyamka, alisema wameendelea kupunguza wafungwa kupitia Sheria ya Parole, pamoja na vifungo vya nje kwa wafungwa ambao wanakidhi vigezo.

Alisema wafungwa wamekuwa wakipewa vifungo vya nje kwa kupewa adhabu za kufanya shughuli za kijamii, wengine kupitia Sheria ya Parole na wengine kupitia msamaha wa Rais imesaidia kupunguza msongamano.

Kadhalika, alisema wamekuwa wakihamisha wafungwa kutoka gereza ambalo lina msongamano na kuwahamishia katika magereza yenye nafasi.

Aidha, alisema wafungwa waliopo kwenye magereza hayo wanahudumiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria za nchini, ikiwamo kurekebishwa tabia kwa kufundishwa stadi za kazi ili wakimaliza vifungo vyao wakaendelee na shughuli za ujenzi wa taifa.

Alisema wamekuwa wakifanya shughuli za kilimo katika magereza ambayo yanaendesha kilimo na ufugaji kwa ajili ya uzalishaji wa mazao mbalimbali pamoja na mifugo.

## LATRA yaadhibu magari 5 kutotumia tiketi mtandao

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), imekamata mabasi matano na kuyatoza faini ya Sh. 250,000 kila moja, kwa kushindwa kuwakatia tiketi za kielektroniki abiria kama sheria zinavyoelekeza.

Ofisa wa LATRA Mkoa wa Singida, Kilua Mbezi, akizungumza na waandishi juzi, alisema mabasi yaliyotozwa faini hizo ni ya Kampuni ya Nyahunge mabasi manne na basi moja la Kampuni ya Super Feo.

Alisema mabasi hayo ambayo yalikuwa yakisafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza yalikumbana na adhabu hiyo kutokana na kuwakatia abiria tiketi za zamani ambazo sio za kielektroniki zilizopigwa marufuku.

Hatua ya LATRA Mkoa wa Singida kuyatoza faini mabasi hayo ilikuja baada ya mmoja wa wasafiri waliokuwa ndani ya mabasi hayo kutoa taarifa kwa Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Singida, Layla Dafa kuwapo kwa abiria waliokatiwa tiketi ambazo siyo za kielektroniki.

Baada ya Dafa kupewa taarifa hizo, alimtuma ofisa wake kuyafutilia mabasi hayo Stendi Kuu ya Mabasi Mkoa wa Singida ya Misuna na kubaini kosa hilo na kuyatoza faini hizo.

# Bodaboda wanaobeba 'mishkaki' hatarini kupoteza nguvu za kiume

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

DAKTARI bingwa wa magonjwa ya mfumo wa mkojo na uzazi wa wanaume katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Remigius Rugakingira, amesema waendesha pikipiki wanaobeba watu zaidi ya mmoja na kukalia tangi la mafuta wapo hatarini kukabiliwa na upungufu wa nguvu za kiume.

Akizungumza na Nipashe, Dk.Remigius alisema licha ya mafuta kuwa na kemikali hata tangi linaloyahifadhi hupata joto, pikipiki ikitembea kwa muda mrefu humuathiri dereva. Alisema hivyo kwa mwendeshaji kukaa juu ya tangi inazidisha kiwango cha joto kwenye korodani ambacho ni kiwanda cha kuzalisha mbegu za uzazi na vichocheo vinavyochangia uume kusimama.

Alibainisha kuwa ingawa utafiti za kisayansi unaonesha kuwapo kwa visababishi mbalimbali vya maradhi ya upungufu wa nguvu za kiume kama mtindo wa maisha hasa ulaji usiyofaa, kutoshughulisha miili na saikolojia ya washiriki wa tendo la ndoa, upo ushahidi wa kisayansi kuwa wanaume wanaofanya kazi katika mazingira ya joto huathiriwa na tatizo hilo.

Kadhali, alisema kundi jingine lililopo hatarini ni vijana wanaovaa nguo za kubana ikiwamo za ndani kwa kuwa wanabana korodani.

Aliwataka vijana kuwa makini na maelekezo wanayopewa na wataalam wa afya ili kuepuka kupata magonjwa ambayo yanatokana na kupanda mshikaki (watu zaidi ya mmoja).

Alisema vijana wote wanaofanya vitendo hivyo wanapaswa kubadilika mapema ili kuepuka kupata matatizo mbalimbali ya kiafya.

Naye, mmoja wa madereva, Julius John, alisema ni vyema elimu kuhusu hilo iendelee kutolewa kwa madereva ili waweze kutambua madhara ya kupakia watu zaidi ya mmoja.

Alisema wengi wao wanakuwa na tamaa ya kubeba abiria wengi lakini wakipewa elimu juu ya suala hilo hakutakuwa na madhara.

John alisema: "Naiomba serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii hususani madereva bodaboda ambao wanapenda kupakiza mishikaki".




Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya tume hiyo na mwelekeo wa utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 jijini Dodoma juzi kwenye ukumbi wa Idara ya Habari (MAELEZO) **PICHA: PAUL MABEJA.**

# JKT latoa hadhari uwapo matapeli nafasi za kazi jeshini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKATI Jeshi la Kujenga Taifa(JKT) limeanza maandalizi ya vijana wa kujitolea kujiunga na jeshi hilo limetahadharisha kuwapo kwa matapeli ambao wamekuwa wakiomba fedha ili kuwatafutia nafasi vijana wao jeshini.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi kwa niaba ya Mkuu wa JKT, Mkuu wa Tawi la Utawala wa JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, alisema utaratibu wa vijana kuomba na kuchaguliwa kujiunga na mafunzo hayo unaratibiwa na ofisi ya za wakuu wa mikoa na wilaya katika eneo analotoka mwombaji.

Alisema maandalizi ya vijana hao kujiunga na

mafunzo hayo ya kujitolea umepangwa kuanza Agosti 28, 2023 (jana) kwa mikoa yote ya bara na visiwani na watakapochaguliwa wataripoti kwenye kambi za jeshi kuanzia Septemba 26 hadi 29, 2023.

"Kumekuwa na wimbi la utapeli unaoendeshwa na baadhi ya watu ambao wakiwaomba fedha vijana wanaoomba nafasi hizo, naomba niwaambie nafasi hizi haziuzwi ni bure hivyo kila mmoja aombe sehemu husika zilizotolewa na JKT," alisema Brigedia Jenerali Mabena.

Aidha, alisema vijana hao ambao watachaguliwa kujiunga na mafunzo hayo, JKT haitoi ajira pia haihusiki kuwatafutia ajira katika asasi na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama bali jeshi hilo hutoa mafunzo kwa ajili ya kuwaandaa vijana kwa ajili ya kujiajiri wao wenyewe.

Alibainisha sifa za waombaji wa nafasi hiyo kuwa ni vijana wa darasa la saba wanapaswa kuwa na umri kuanzia miaka 16 hadi 18 ambao wamemaliza elimu ya msingi kuanzia mwaka 2020 hadi 2022,wakati waliohitimu kidato cha nne wanapaswa kuwa na umri usiozidi miaka 20 na awe na ufaulu kuanzia daraja la kwanza hadi la nne na ufaulu uwe kuanzia alama 26 hadi 32.

Pia, alisema kwa waliohitimu kidato cha sita wawe na umri usiozidi miaka 22 ambao wamemaliza kuanzia mwaka 2020 hadi 2022 na awe na cheti chenye ufaulu wa kuanzia daraja la kwanza hadi la nne.

"Waombaji wasiwe wametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) wala kuajiriwa na idara nyingine serikalini,"alisema.

Kadhalika, alitoa onyo kwa watakaokutwa na nyaraka za kughushi watachukuliwa hatua kali za kisheria.



# Wazazi wanyooshewa kidole mmomonyoko wa maadili

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZAZI na walezi wametakiwa kushiriki katika kukabiliana na matatizo ya mmomonyoko wa maadili kwa watoto yanayotokana na mabadiliko ya teknolojia kwa kukaa nao na kuwaeleza ukweli kuhusu mambo hayo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi Maalumu, George Mkuchika aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kufunga Tamasha la Pili la Kitaifa la Utamaduni ambalo lilifanyika mkoani Njombe.

Waziri Mkuchika alisema: "Hivi sasa wanafahamu kupitia mitandao ambayo ipo kwenye viganja vyao ninaomba kuwasihi wazazi wenzangu tujitahidi kukaa na watoto wetu na kuongea nao ukiacha kumwambia kwa kudhani ni mdogo ataambiwa na dunia kupitia vyombo".

Alisema kuwa hatari kubwa ni kuwepo kwa tamaduni za kigeni kutaka kumeza tamaduni zetu kwa kigezo cha kulazimisha baadhi ya mambo kwa kutumia jina la haki za binadamu.

"Hapa nataka kuzungumza hili janga balaa la ushoga linalotoka nchi za nje, ushoga mume kuoa mume mwenzako, mama kuoa mke mwenziwe, mzee mwinyi alihojiwa juu ya hili nimependa alisema hivi hata wanyama hawafanyi hivyo, wanyama wanaakili kushinda binadamu umeona lini mbwa dume na mbwa dume sasa wenzetu wa nje wanasema ushoga ni haki za binadamu, haki binadamu kumuumiza dume mwenzio au umeona wapi mwanamke anazaa na mwanamke mwenzake" alisema Mkuchika.

Pia, aliitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuhakikisha wanadhibiti mambo yanayokiuka misingi ya maadili katika mitandao ili kusaidia taifa lisiangamie.

Alisema mamlaka hiyo ya mawasiliano ni wadau muhimu wa kuhakikisha maadili yanalindwa.

"Naomba nitumie fursa hii kuwaomba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kudhibiti mambo yanayokiuka misingi ya maadili katika mitandao" alisema Mkuchika.

Hata hivyo alizitaka taasisi za kijamii kuanzia ngazi za kifamilia na mashirika kutoa mafunzo kwa vijana kuhusu mila, desturi na utamaduni wa Tanzania.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Rebbeca Nsemwa ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, alisema kuwa Watanzania wakiendelea kujiingiza katika masuala ya ushoga tutashindwa kuwa na taifa endelevu.

"Hatuwezi kupata taifa endelevu kwa kuoana mwanaume kwa mwanaume au mwanamke kwa mwanamke na sisi tunategemea taifa letu liendelee kukua kwa population (idadi ya watu) hivyo tukiendekeza mambo ya ushoga hatutakuwa na taifa endelevu hapo baadae" alisema Nsemwa.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe alisema kupitia tamasha hilo wamepata faida nyingi kwani biashara kubwa zimefanyika kutokana ujio wa watu wengi kutoka mikoa tofauti nchini.

Mwakilishi wa UNESCO nchini, Nancy Mwaisaka alisema shirika hilo linaihakikishia serikali kuendelea kufanya kazi bega kwa bega katika kulinda na kuendeleza utamaduni wa mtanzania.



Gari likiwa limeacha njia na kuingia mtaroni eneo la Kimara Bucha Dar es Salaam jana. Kwa mujibu wa mashuhuda, dereva alikuwa akikwepa kugonga gari iliokuwa mbele kusubiri taa ziruhusu kupita. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Walimu wapewa jukumu kukomesha vitendo vya ukatili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WALIMU mkoani Mbeya wametakiwa kusaidiana na wazazi kwenye malezi ya watoto ili kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya kundi hilo ambavyo vimekuwa vikitokea mara kwa mara mkoani humo na kuathiri mfumo wa maadili.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye kongamano maalumu la walimu lililoandaliwa na Benki ya NMB kwa lengo la kutoa elimu kuhusu huduma mbalimbali zilizoanzishwa kwa ajili ya walimu kupitia kifurushi cha 'Mwalimu Special'.

Kongamano hilo liliwashirikisha walimu wakuu wa shule za msingi, wakuu wa shule za sekondari, maofisa elimu na baadhi ya viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Mbeya.

Malisa alisema walimu ndio kundi ambalo linakaa na watoto kwa muda mrefu kuliko hata wazazi na hivyo akawaomba kusaidia kuwalea watoto hao kwenye maadili mema ili kuwaepusha na vitendo hivyo vya ukatili.

"Juzi juzi huko Isanga kuna mtu ambaye alikuwa hafahamiki, alimlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka mitano na kumsababishia kifo, bahati mbaya ni kwamba wananchi nao walijichukulia sheria mkononi kwa kumpiga mpaka wakaua na kumchoma moto," alisema Malisa na kuongeza.

"Nyinyi ni watu muhimu sana kwenye malezi ya watoto, tunaomba sana mtusaidie kuwaelewesha watoto kuhusu masuala ya maadili ili tuwe na kizazi cha baadaye kizuri," aliongeza.

Meneja Mwandamizi wa Wateja Binafsi wa NMB, Ally Ngingite alisema lengo la kongamano hilo ilikuwa ni kuwaelimisha walimu kuhusu matumizi ya huduma mbalimbali za kibenki ambazo zimeanzishwa maalumu kwa ajili ya kundi hilo.

Alisema kupitia kifurushi cha 'Mwalimu Special' walimu wanapata mkopo wa kujiendeleza kielimu ambao unafika mpaka Sh. milioni 10 na kwamba mkopo huo hauna masharti magumu kama ilivyo kwa mikopo ya makundi mengine.

Alisema mwalimu anapewa mkopo huo baada ya kupata chuo huku akisisitiza kuwa mkopo huo unahusika pia kuwasomesha wategemezi wa mwalimu husika wakiwemo watoto kuanzia ngazi ya awali mpaka chuo kikuu.

Vilevile alisema kifurushi hicho pia kinatoa huduma ya mkopo wa vyombo vya moto kwa walimu ambavyo ni pikipiki na bajaji kwa ajili ya kuendeshea shughuli za ujasiriamali.

"Mikopo hii yote mwalimu anapata kwa asilimia 100 bila masharti ya kuweka kianzio, anakuwa anarejesha kidogokidogo mpaka atakapomaliza, lakini akikopeshwa pikipiki ama bajaji tunamfungia mfumo maalumu wa ufuatiliaji ili kudhibiti wizi na matumizi mabaya," alisema Ngingite. Vilevile alisema walilenga kuwafundisha walimu huduma zingine za benki hiyo ikiwemo kujiwekea akiba, kupata mikopo midogo midogo inayopatikana kupitia NMB mkononi.

Baadhi ya walimu walioshiriki kongamano hilo walisema elimu waliyoipata itawasaidia kubadili maisha yao ikiwa ni pamoja na kuacha kuchukua mikopo kwenye taasisi zisizokuwa rasmi ambayo imekuwa ikiwaumiza.

Mmoja wa walimu hao, Juliana Ndingwango alisema baadhi ya walimu wamekuwa wakijiingiza kwenye mikopo umiza bila wao wenyewe kujua na hivyo kurudisha maisha yao nyuma.

# Vijana watakiwa kurasimisha kazi ili kujiendeleza kibiashara

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

VIJANA mkoani Njombe wametakiwa kurasimisha kazi zao za sanaa pamoja na vitu walivyovibuni ambavyo vitaweza kuwasaidia kibiashara na kuweza kuendelea.

Ushauri huo ulitolewa na msaidizi wa usajili mwandamizi mkurugenzi wa miliki bunifu (BRELA), Nassoro Mtavu kwenye tamasha la pili utamaduni kitaifa mkoani Njombe.

Mtavu alisema kuwa vijana wengi wanajiingiza katika sanaa lakini wanakuwa na vitu ambavyo hawajavirasimisha.

"Wito wangu kwa vijana na watu wengine wote ambao wanatembelea maeneo haya ni kuhakikisha wanakuja katika banda letu na wanapata elimu, hapa tulipo tunatoa huduma zote ambazo zinaweza kutolewa makao makuu mfano usajili wa kampuni, usajili wa majina ya biashara, usajili wa alama za bidhaa na huduma, leseni za viwanda, leseni za biashara vile vile daraja A kama ambavyo sheria inatutaka tufanye" alisema Mtavu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, Nyakaho Mahemba, alisema mfuko huo upo kwa ajili ya kutatua changamoto ya mitaji kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wasanii.

"Mfuko huu unatoa mikopo kwa kikundi, kampuni na mtu mmoja mmoja na kiwango cha mkopo ni Sh. 200,000 mpaka Shilingi milioni moja," alisema Mahemba.

Ofisa Utalii kutoka Bodi ya Utalii Tanzania TTB, Hozza Mbura alisema bodi hiyo imepewa majukumu ya kutangaza utalii Tanzania na vivutio vinavyopatikana kusini mwa Tanzania.

"Bodi ya utalii imekuwa ikishiriki maonesho mbalimbali ya kimkakati ili kutoa taarifa za utalii pamoja na kuhamasisha wadau, watu kutembelea vivutio kwa hiyo tamasha hili ni fursa,"alisema Hoza.

Awali Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dk.Pindi Chana, alitoa wito kwa wasanii kuendelea kujisajili kupitia Baraza la Sanaa ili waendelee kunufaika na mikopo inayotolewa na serikali.



## TAMWA yapongeza wanawake kuteuliwa Tume ya Uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, (TAMWA- Zanzibar) kimefurahishwa na uteuzi wa muundo wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Kimesema hatua ya wanawake wawili kupata uteuzi akiwemo Jaji Aziza Iddi Suwedi na Halima Mohamed Said kwa kuteuliwa kuwa wajumbe wa tume hiyo.

Pongezi hizo zimekuja kufuatia uteuzi uliofanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi hivi karibuni baada ya kuwateua wajumbe wapya wa tume hiyo yenye jukumu la kusimamia uchaguzi mkuu wa Zanzibar.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Mkurugenzi wa TAMWA, Zanzibar Dk. Mzuri Issa, alisema Tume ya Uchaguzi imehusisha wajumbe saba, watano wakiwa ni wanaume akiwemo Mwenyekiti Jaji George Joseph Kazi, hivyo kuwa na wanawake wawili sawa na asilimia 28.6 na wanaume kuwa ni asilimia 71.4.

"TAMWA inawatakia kila la kheri wajumbe hao wanawake na kuwaomba wasimamie maslahi ya wanawake katika uchaguzi ikiwemo kuweka mifumo ya kuripoti udhalilishaji/ukatili wa wanawake katika siasa, usalama wa wanawake katika uchaguzi na kupinga vita masuala ya rushwa na matumizi mabaya ya fedha katika uchaguzi"alisema Dk. Mzuri.

Alisema Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Tanzania imeridhia mikataba mingi ya kikanda na kidunia, kuleta usawa wa kijinsia katika vyombo vya maamuzi.

Alisema ni muhimu kwa mamlaka za uteuzi kuhakikisha kuwa zinateua wanawake na wanaume kwa usawa wa 50/50 ili kufikia usawa wa kijinsia.

# THRDC yakabidhi mwongozo utoaji malalamiko wafungwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umekabidhi muongozo wa utoaji wa malalamiko na mawasiliano kwa wafungwa na watuhumiwa waliopo mahabusu katika magereza ya Zanzibar.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya muongozo huo iliyofanyika makao makuu ya Chuo cha Mafunzo Zanzibar (Magereza), kuambatana na uwekaji wa visanduku vya maoni, Naibu Kamishna wa chuo hicho, Haji Hamdu, alisema mwongozo huo ni muhimu katika kutekeleza matakwa ya haki za binadamu kimataifa.

Kadhalika, aliahidi kuifanyia kazi miongozo hiyo kwa sababu dhana ya zamani ya kwamba wafungwa kupewa adhabu ngumu wameshaondokana nayo gerezani hapo.

"Tunawahidi kwamba miongozo iliyomo humu tutaendelea kuitumia na fursa za wafungwa kutoa maoni yao itapatikana na kufanyiwa kazi ili kuwa na mabadiliko makubwa katika utekelezaji wa haki za binadamu" alisema.

Alisema maoni yote yatakayotolewa na wafungwa na mahabusu gerezani hapo hayatachujwa bali yatachambuliwa na kufanyiwa kazi ili haki ipatikane.

Naye Mkuu wa Idara ya Sheria na Urekebishaji wa Magereza, Kamishna msaidizi Seif Mabadi Makungu, alisema awali utoaji wa malalamiko utaratibu wake haukuwa rasmi na baadhi ya wakati malalamiko huchukua muda katika kuchukuliwa hatua.

Alisema mwongozo huo mpya uliowasilishwa utasaidia kuimarisha ustawi, mahitaji na fursa ambazo zimewekwa kisheria kwa waliowekwa mahabusu zinapatikana.

Aidha, alisema kuna tatizo la waliopo mahabusu kupata mawasiliano kutoka kwa ndugu zao, hivyo chuo cha mafunzo kinafanya marekebisho ya kisheria ili kwenda na wakati na teknolojia katika kuimarisha huduma ili wafungwa na mahabusu kuwasiliana na jamaa zao.

Mratibu wa (THRDC) Zanzibar, Suleiman Ujuni Baitani, alisema lengo la kushirikiana na Jeshi la Magereza ni kuhakikisha kuimarisha ushirikiano na haki za binadamu zinaheshimiwa, zinalindwa na kutetewa kwa wafungwa na mahabusu waliopo magereza kwa kuwasilisha malalamiko yao na kufanyiwa kazi.

Alisema miongoni mwa mwongozo huo ni kuhakikisha wadau wa haki za binadamu wanashirikiana na Jeshi la Magereza katika kuhakikisha mazingira salama, kuikumbusha serikali kuendelea kusimamia, kulinda na kuheshimu mikataba ya kimataifa ili kuhakikisha haki za binadamu zinathaminiwa.

"Mahabusu na wafungwa waliopo magerezani wana uwezo wa kulalamika lakini pia kuhakikisha haki zao zinasimamiwa," alisema.

Wakizungumza katika hafla hiyo, wafungwa na mahabusu waliopo gerezani hapo, walisema hawaridhishwi na usikilizaji wa kesi mahakamani hali ambayo imesababisha kukaa mahabusu kwa muda mrefu bila ya kesi kutolewa hukumu.

"Nipo mahabusu huu ni mwezi wa nane kesi yangu haijaanza kusikilizwa tunaiomba serikali iharakishe usikilizaji wa kesi mahakamani ili kama nina hatia nipewe adhabu inayostahiki kuliko kuwekwa kizuizini muda mrefu wakati nina familia inanitegemea" alisema mmoja wa mahabusu ambaye hakutaka kutaja jina lake liandikwe.

Mahabusu mwingine, Jafet Frank, anaetumikia kifungo gerezani alisema wamepoteza mawasiliano na ndugu zake kwa sababu wanapoingia gerezani hupoteza vitu vyao vya thamani ikiwemo simu na kukosa mawasiliano.

Alisema: "Mimi kwetu Shinyanga na mwakani namaliza kutumikia kifungo lakini sina mawasiliano na ndugu zangu hata nikitoka hapa gerezani, sijui pakuazia ili kufika kwetu".

Mfungwa mwingine, Samuel John, alisema kuna changamoto ya usikilizaji wa kesi na utoaji wa hukumu katika Mahakama ya Rufani Tanzania ambapo mchakato wake huchukua muda mrefu wakati rufaa ni haki ya kila mshtakiwa.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa tatu kulia), akimsikiliza Mhandisi Fatma Kara (aliyeshika kipaza sauti), akitoa ufafanuzi kuhusu mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kizimkazi kilichopo Mkoa wa Kusini Unguja kinachojengwa na serikali kwa kushirikiana na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ikiwa ni sehemu ya uzinduzi wa Tamasha la Kizimkazi 2023. Wengine ni Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Hafidh (wa nne kulia), Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (wa pili kulia), Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (katikati). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wimbi la utoaji talaka laishtua Baraza la Maulamaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kudhibiti matukio ya utoaji talaka, Baraza la Maulamaa Zanzibar limetakiwa kutoa elimu ya ndoa kwa jamii ili wanandoa kuepuka migogoro inayosababisha kuvunjika kwa ndoa.

Ushauri huo umetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akizungumza na Baraza la Maulamaa pamoja na watendaji wa ofisi ya Mufti katika ziara ya kutembelea taasisi ziliopo chini ya wizara yake.

Alisema jamii hivi sasa inashuhudia kuporomoka kwa maadili ambayo yamechangiwa na kuwepo kwa malezi duni kutoka kwa familia pamoja wazazi wawili baba na mama.

Suleiman alisema miongoni mwa sababu zinazosababisha wimbi la takala na kuvunjika kwa ndoa ni kuporomoka kwa maadili katika jamii.

Aidha, aliitaka Ofisi ya Mufti pamoja na Baraza la Maulamaa kutoa elimu zaidi kupitia vyombo vya habari kuhusu malezi ni utamaduni wa Zanzibar na kuepuka upotoshaji unaofanywa wa kuingiza tamaduni za kigeni.

"Baraza la Maulamaa tunakabiliwa na changamoto kubwa ya kuporomoka kwa maadili ya vijana wetu ambapo matokeo yake ndoa zinavunjika katika kipindi kifupi sasa huu ni wakati wa kutusaidia kulipatia ufumbuzi tatizo hilo"alisema.

Naye, Katibu Mtendaji kutoka Ofisi ya Mufti Zanzibar, Shekhe Khalid Mfaume, alisema wameanza kutoa elimu ya mafunzo kwa walimu wa madrasa, kuona kwamba wanatekeleza majukumu yao vizuri na kuepuka matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema wamekamilisha mchakato wa kufanya usajili wa vyuo vyote vya madrasa kwa ajili ya kuvitambua na kuweka mitaala ya kufundishia masomo yake.

"Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar tumekamilisha kazi ya kufanya usajili wa vyuo vya madrasa kwa ajili ya kuvitambua na kuweka utaratibu wa mitaala ya kufundishia wanafunzi" alisema.

Mjumbe wa Baraza la Maulamaa, Shekhe Khamis Abdulhamid, alisema utandawazi umeleta mabadiliko makubwa ya maisha ya vijana kwa kuiga mila za kimagharibi.

Alisema "Faida za utandawazi na dunia kwa ujumla ndiyo tunaziona kwa sasa ambapo tunashuhudia vijana wetu kubadilika na kuiga tamaduni za Ulaya".

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**AIRENE DASTAN RAPHAEL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1406/0003/2019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **JAMHURI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/PWA/MKU/193/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACOB J. NGOLO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0740/0111** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ALI HASSAN MWINYI SECONDARY SCHOOL** TABORA mwaka 2009. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **TAB/RB/1926/2016**

## DEED POLL OF CHANGE OF NAME



**BY THIS DEED, I, ESTER DAUDI MTOI** adult, Christian and resident of Lushoto,Tanzania DO HEREBY wholly absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of the name **ZULEKHA DAUDI** formerly used before getting marriage and also used in my PSPF records and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of the name of **ESTER DAUDI MTOI** as appearing in my certificate of birth with registration **No.02690203 and NIDA No.19770316217140000115.** This is so because the use of the two names to refer to one person has been prone to confuse, hence this deed poll to rectify the situation.

Forthe purpose of evidence of such determination I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deed documents and other writtings and in all actions, suits and proceedings as well as in all public and private dealings and transactions and occasions whatsoever use, subscribe the name of **ESTER DAUDI MTOI** as my name in lieu of and substitution for the name **ZULEKHA DAUDI.**

I hereby expressly authorize and require all and every person and whosoever at all times after the date hereof to designate, describe and address me by the name of E**STER DAUDI MTOI.**

**IN WITNESS WHEREOF I** herein substitute the names **ESTER DAUDI MTOI** by the names of **ZULEKHA DAUDI** and have set my hand at Lushoto this 10th day of August, 2023.

Dated at Lushoto this 10th day of August,2023.

SIGNED and DELIVERED by the said ESTER DAUDI MTOI who is known to me personally/ identified to me by ........................the latter being known to me personally in my presence this 10th day of August, 2023.

.................... DEPONENT



BEFORE ME:
Name: ALLY JUMAA KIMWERI
Signature:...................
Address: P. O. Box 36, Lushoto-Tanga.
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS

Ally Jumaa Kimweri
P.O Box 36 Lushoto
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## MAHAKAMA

**FORM II**

**SMM 1994 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya mwanzo ya Mwambao wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa pwani. Ombi la ndugu **MWANAHAMISI RASHID KISOME** kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi namba 54/2023 ya marehemu **RASHID IDD KISOME** watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi hii wakitaka mnamo tarehe 14/9/2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hii.

Wosia wa Marehemu **HAKUNA WOSIA**

SAHIHI YA HAKIMU

TAREHE: 25/8/2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MWAMBAO - BAGAMOYO

## KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA

**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SAHURI LA MADAI NAMBARI .....64......LA 2022**
**DR. JOHN RAPHAEL NYIKA .....................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1) **WILLIAM MATO**
2) **REGISTERED TRUSTEES OF CHAMA CHA MAPINDUZI...........................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1) **WILLIAM MATO**
2) **REGISTERED TRUSTEES OF CHAMA CHA MAPINDUZI**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**DR. JOHN RAPHAEL NYIKA** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 13/9/2023 saa 03:00 Asubuhi/mchana mbele ya Mh J.W.SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 21 Mwezi 08...2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## IN THE DISTRICT COURT OF MOSHI AT MOSHI

**CIVIL CASE NO.10 OF 2023**

**JUBILATE NASRI SWAI.................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**VICENT JOHN MMASI.................................DEFENDANT .**

**NOTICE FOR MENTION,**

**TO VICENT JOHN MMASI**
**C/O MWENYEKITI WA MTAA KIBOSHO ROAD AREA**

**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for mention in the DMS Court at Moshi on 7 the day of 09 ,2023 at 9:00 a.m. Oclock in the forenoon.

You may appear in person or by Advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day of document under which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE that:** default of your appearance on that day before mention the court will proceed with the matter in your absence.

A copy of the petition and are attached here to.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 3 rd day of 08, 2023

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
MOSHI

## IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 93/ 2023**

**In the matter of the Estate of the late MELEYA MASAKA MLEMETHA of KIKOMBO within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANA YONA NELSON YUSUPHU**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 29 Day of 8,2023

**Date at Dodoma this 28 Day of JULY 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

## IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 92/ 2023**

**In the matter of the Estate of the late BENEDICTO EMMANUEL BUGUFI of SWASWA within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SYLIVIA KEMILEMBE BENEDICT**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 29 Day of 8,2023

**Date at Dodoma this 31 Day of JULY 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE I/C
DODOMA DISTRICT

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA/ KIMATAIFA

# Upinzani Zimbabwe wapinga ushindi rais mteule

**HARARE,** Zimbabwe

UPINZANI nchini Zimbabwe umeyapinga matokeo ya uchaguzi mkuu yaliyomrejesha madarakani Rais Emmerson Mnangagwa wa Chama Tawala cha (ZANU-PF), ukieleza kuwa hauyatambui kwa kuwa mchakato wa uchaguzi ulijaa hila na udanganyifu.

Pingamizi hilo limekuja saa chache baada ya ubalozi wa Marekani mjini Harare kujiunga na waangalizi wengine wa uchaguzi huo na kueleza wasi wasi wao kwamba haukufikia viwango vya katiba ya nchi hiyo na miongozo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Chama kikuu cha upinzani nchini Zimbabwe cha CCC kilitangaza msimamo wa kuyapinga matokeo hayo ya uchaguzi jana baada ya Tume ya Uchaguzi ya taifa hilo kumtangaza Rais Mnangagwa kuwa mshindi wa uchaguzi huo uliofanyika Jumatano ya wiki iliyopita.

Matokeo ya tume yalionyesha kiongozi huyo wa chama cha ZANU-PF alishinda muhula mwingine madarakani kwa kupata asilimia 52.6 ya kura dhidi ya mwanasiasa wa upinzani Nelson Chamisa aliyepata asilimia 45.

Katika tamko la kwanza tangu kutolewa matokeo hayo, Chamisa aliandika matamshi makali ya kuyapinga kupitia ukurasa wa mtandao X uliofahamika zamani kama Twitter, akisema watayapinga matokeo kwa nguvu kubwa. Alisema matokeo ya uchaguzi huo yamechakachuliwa na wananuwia kuyapinga kisheria, akieleza kuwa kazi ya kuhesabu na kuyajumlisha matokeo haikufanyika kwa usahihi.

Sehemu ya ujumbe wa Chamisa, ilisema "wameiba sauti na kura zenu lakini kamwe siyo matumaini yenu hatutanyamaza".

"Mabadiliko yanakuja Zimbabwe iwe chama cha ZANU-PF kinyataka au hakiyataki, haitokuwa rahisi lakini mabadiliko yanakuja, hatutasubiri miaka mingine mitano, mabadiliko lazima yatokee sasa na tutakuwa mstari wa mbele kuhakikisha mabadiliko yanatokea Zimbabwe, ni lazima tukomeshe uwendawazimu huu," alisema Chamisa.

Ilielezwa kuwa haijafahamika mara moja ni vipi Chamisa analenga kutimiza lengo hilo la mabadiliko lakini mpinzani wake aliyetangazwa mshindi Rais Mnangagwa aliwakosoa wanaoyapinga matokeo ya uchaguzi, huku akikuwakumbusha kuwa wanayo haki ya kwenda mahakamani. Katika ujumbe alioutoa baada ya kutolewa matokeo Mnangagwa aliusifu uchaguzi huo kuwa wa kihistoria na kuahidi kufanya kazi kwa bidii katika muhula mpya wa utawala wake.

"Hakuna washindi na walioshindwa, lakini kuna taifa moja tu la watu wa Zimbabwe walioungana. Kwa jumla tumewaibisha wabaya wetu waliotamani kutuona tunagawanyika na kutumbukia kwenye machafuko. Daima tutabakia wamoja, wapenda amani na watu wastahamilivu," alisisitiza Mnangagwa.

Licha ya msisitizo huo wa rais Mnangagwa, ilielezwa kuwa uchaguzi huo wa rais na bunge ulishuhudia dosari kadhaa siku ya upigaji kura, ikiwemo ucheleweshaji kufunguliwa vituo vya kupigia kura na madai ya ukandamizaji wa wapiga kura. Katika baadhi ya wilaya uchaguzi ulilazimika kufanyika siku iliyofuata na kwamba changamoto hizo ndiyo zimefanya timu za waangalizi wa kikanda na kimataifa kuhitimisha kuwa uchaguzi wa Zimbabwe haukukidhi viwango vya kimataifa.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterress naye alizungumzia mashaka yake baada ya kuwapo taarifa za kukamatwa kwa waangalizi, vitisho kwa upinzani na wapigakura. **DW**



Wafuasi wa ZANU-PF wakishangilia ushindi wa matokeo ya urais. **PICHA: REUTERS**

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Shahidi: DCI hakuridhishwa upelelezi, aliongeza nguvu

**Na Grace Gurisha**

MKUU wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, David Mwanahe (56), amedai mahakamani kuwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Athumani Diwani hakupendezwa na upelelezi wa tukio la mauaji ya Aneth Msuya, mdogo wa marehemu Erasto Msuya 'maarufu Bilionea Msuya', hivyo akalazimika kuongeza nguvu kutoka ofisini kwake.

Vilevile, mahakama imeelezwa kuwa binti wa kazi wa Aneth, Getruda Mfuru, alionesha Sh. milioni 50 zikiwa kwenye mkoba na mwanamke aliyemtambua kama mke wa Erasto na kuelezwa kuwa ni za kwake baada ya kazi kuisha, lakini baadaye alipewa Sh. 20,000.

Mwanahe alidai hayo mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi katika kesi hiyo, akiongozwa na Wakili wa Serikali, Paul Kimweri.

Alidai kuwa Julai 12, 2016, saa nne asubuhi, alikuwa ofisini kwake, Makao Makuu ya Upelelezi ya Makosa ya Jinai, Dar es Salaam, yeye na ASP Jumanne waliitwa na DCI Diwani kwa ajili ya kwenda kufanya upelelezi wa kesi ya mauaji ambayo ilikuwa inapelelezwa na RCO Temeke, mauaji ya Aneth Msuya.

Alidai DCI Diwani aliwaeleza kuwa hakupendezwa na upelelezi wa tukio hilo. Alitoa maelezo kwa ASP Jumanne kwamba aandae timu watakayokwenda nayo kwa RCO Temeke.

Shahidi huyo wa 22, alidai Jumanne aliandaa timu ya askari wanne na dereva mmoja, baada ya kukamilika kwa timu hiyo, DCI aliwapa maelezo wakaripoti kwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kipolisi Temeke kwa SSP Mchovu.

Alidai kuwa Julai 25, 2016, aliitwa na SSP Mchovu na kuelezwa kuwa dada wa kazi wa Aneth, Getruda Mfuru aliyetoweka kabla ya tukio kutokea, amepatikana, alimtaka WP Esther akamlete binti huyo ili akiwa anamhoji, naye awapo.

SSP Mwanahe alidai alimhoji binti huyo kwa saa moja na nusu. Alikuwa na wasiwasi na aliomba wamlinde.

"Nilimwondoa shaka na akaridhia kunielezea yaliyojiri na kusababisha yeye kuondoka nyumbani kwa Aneth Msuya kabla ya kutokea tukio hilo," alidai SSP Mwanahe.

Alidai kuwa alianza kumweleza kwamba Mei 15, 2016, saa tisa na nusu kuelekea saa 10 alikuwa akitokea nyumbani kwa Aneth akielekea dukani kununua tishu (toilet paper), alikutana na gari aina Ford Range lenye rangi bluu nyeusi. Lilisimamishwa na kioo kikafunguliwa. Akamwona mama mnene mwenye uso wa mviringo, mweupe, akamsemesha kwa kumsalimia.

Pia alidai kuwa kwenye gari hilo kulikuwa na mwanamume ambaye alikuwa akiendesha gari hilo. Mama huyo alimwuliza 'kwa Aneth Msuya ni sehemu gani? Akamwonesha kwa ishara ya kidole.

"Huyo mama akamuuliza kwa sasa hivi yupo? Akamjibu 'bado hajarudi kazini'. Akamwambia 'basi kuna kazi ninataka kufanya na wewe, lakini hakumweleza ni kazi gani. Akamwambia angekuja siku iliyofuata, lakini akamtaka awe msiri, asimwambie mtu," alidai

Alidai kuwa Mei 18, 2016, asubuhi binti alimweleza kuwa alikuwa anachota maji ya nyumbani kwao na alipofika mlangoni akiwa na ndoo kichwani ili aingie ndani aliona gari la kifahari na nje ya gari, pembeni alimwona huyo mama aliyemsimamisha siku ya kwanza.

Alidai kuwa mama huyo alikuwa amevaa sketi ya kimini na viatu vya rangi ya zambarau, mwanamume alikuwa amevaa suti nyeusi ndani shati jekundu na viatu vyeupe huku akiwa ameshika mkoba, alimtaka aingie ndani ya gari.

"Alipoingia alikuta watu watatu kwenye siti ya nyuma. Kwa hiyo, jumla kwenye gari walikuwa sita, watu hao walikuwa wameficha sura wanaonekana mdomo na macho na alipokuwa akiwaangalia mmoja alitoa bastola na kumwekea begani.

"Yule mama akatoa sauti ya ukali kwamba 'wewe usiangalie nyuma, niangalie mimi, mali nitafute mimi wengine wazitumie. Yule mwanamume alikuwa kwenye usukani akaguna, ndipo huyo mama akatoa simu ndogo aina ya Nokia, akampa huku akimweleza kwamba kuna laini ya Airtel," alidai.

Alimweleza kuwa anampatia simu hiyo kwa ajili ya kufanya naye mawasiliano na kumwonya asimwoneshe mtu na watakuwa wanamfuatilia, akamwonesha mkoba wenye fedha na kumwambia 'hizo ni Sh. milioni 50 ni za kwako kama kazi hiyo ikifanikiwa'.

Alidai kuwa Mei 18, 2016, binti huyo alipomwona mama huyo, alimwuliza kwa ukali kama anamfahamu, akamjibu kwamba hamfahamu, lakini kuanzia hapo baada ya sauti hiyo ya ukali akaanza kuvuta kumbukumbu.

"Alikumbuka kuwa alimwona Mirerani wakati akifanya kazi kwa Bibi Msuya ambaye ni mama yake Aneth. Mei 23, 2016, alipigiwa simu na huyo mama akataka waonane, ambapo siku hiyo walisimama kama mita 200 kutoka kwa Aneth.

"Yeye akiwa ameegemea kioo alipewa maelezo kwamba kabla ya tarehe 25 awe ameondoka hapo na kumsisitiza simu waliyompa aiharibu ili mtu yeyote asimpate. Aliingiwa na woga na alipatiwa Sh. 20,000 kwa maelezo itamsaidia," alidai.

Alidai kuwa ilipofika Mei 25, 2016, asubuhi alifungua mlango wa nyumbani akaweka ufunguo chini ya kapeti la nje na ufunguo wa geti aliondoka nao kuelekea Feri ambako alikwenda kukutana na mpenzi wake, Samweli Kombo.

Alidai kuwa aliponda pantoni alikumbuka maelekezo ya simu, ndipo alipotupa simu hiyo kwenye maji, alifanikiwa kukutana na mpenzi wake huyo akamweleza kuwa kwa siku hiyo atakuwa mgeni wake, basi wakapanda bodaboda 'mishikaki' hadi karibu na nyumba ya Aneth.

Alidai kuwa kwa mbali aliona gari la Aneth, ndipo akamtafuta mwanafunzi akampa funguo na kumwelekeza aupeleke nyumba ya jirani. Mei 26, 2016 alipigiwa simu na ndugu yake Neema anayeishi Mirerani na kumweleza kuwa Aneth ameuawa kinyama na yeye anatafutwa.

"Ndipo alipoamua kumweleza mpenzi wake, akamshauri kwamba aende polisi, lakini yeye aliogopa akamwomba amtafutie nauli ili arudi nyumbani, alimtafutie Sh. 50,000, akarudi Moshi nyumbani kwao," alidai.

Katika kesi hiyo, Miriam Mrita, ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni, Dar es Salaam, amekiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo. Mshitakiwa mwingine ni Revocatus Muyela.

# MANDONGA CHALI, CLASS, DULLAH MBABE WAACHA HISTORIA Z'BAR

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Ibrahim Class na Dullah Mbabe, wamefanikiwa kuweka historia mpya mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, kwa kushinda mapambano ya ufunguzi kwa KO na TKO huku Karim Mandonga akichezea kichapo tena.

Katika pambano hilo ambalo lilifanyika juzi, Jumapili kwenye Uwanja wa Mao Tse Tung visiwani Zanzibar, ni uzinduzi wa mchezo huo ambao ulifungiwa kwa kipindi cha miaka 60 kabla ya kufunguliwa kwenye uzinduzi huo na Dk. Hussein Mwinyi.

**Ibrahim Class alicheza pambano kuu na Hamisi Muaithai ambapo alimtandika kwa TKO katika raundi ya saba baada ya Muathai kuamua kuacha mwenye kutokana na kichapo kizito alichokuwa anapokea.**

Class alicheza katika moto wa kawaida hakutaka kuonesha uzito mkubwa kwa mpinzani wake kutokana na kucheza katika kiwango cha chini kilicholalamikiwa na mashabiki wengi kabla ya mpinzani wake kuacha pambano kwenye raundi ya saba.

Kwa upande wa Dullah Mbabe, ilimchukua raundi moja peke yake kumaliza pambano kwa kumchakaza vibaya, Ally Banja kwa KO.

Naye bondia mwenye mbwembwe na maneno mengi, Mandonga, alipanda ulingoni dhidi ya Muller JR katika pambano lililokuwa na ushindani mkali kutoka kwa mabondia hao kuonesha uwezo mkubwa ambapo Mandonga alionekana kuwa bora tofauti na mapambano yake mawili yaliopita ambayo yote alipoteza dhidi ya Daniel Wanyonyi wa Kenya na Moses Golola wa Uganda, hata hivyo alikuwa ni Mulle JR aliyeibuka mshindi kwa pointi kutoka kwa majaji wote watatu.

Mapambano mengine ya utangulizi yaliyopigwa siku hiyo, Sebastian Cosmas na Masudi Hamisi lilimalizika kwa sare ya kiufundi kwenye raundi ya kwanza baada ya kupasuana vichwa wakati Hassan Salum akifanikiwa kumchapa Alli Mkojani huku Said Salum akimchapa Abdallah Selem.

Mara baada ya pambano hilo, Mandonga alimshukuru Rais Dk. Mwinyi, kwa kuweza kuruhusu mchezo huo kuchezwa visiwani Zanzibar huku pia akimpongeza mpinzani wake kwa ushindi.

**PAGAWISHA...**



Mwanamuziki Khaleed Ramadhan maarufu Tunda Man, akiwapagawisha wanafunzi wa Shule ya Sekondari Brilliant wakati wa mahafali ya kidato cha nne, yaliyofanyika shuleni hapo Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Pluijm aukubali muziki wa JKU CAF

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kusonga mbele na kutinga raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho barani Afrika juzi, Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, ameshangazwa na uwezo mkubwa ulioonesha na wapinzani wao, JKU akisema kila muda walivyozidi kwenda ndivyo walivyozidi kuwa hatari kwao.

Hata hivyo, ilibidi Singida Fountain Gate wasubiri filimbi ya mwisho ya mwamuzi ndiyo walipojihakikisha kuwa wametinga hatua inayofuata, huku ikiwa imechapwa mabao 2-0 dhidi ya JKU ya Zanzibar ambayo iliingia kivingine kwenye mechi hiyo ya mkondo wa pili wa hatua ya awali ya kombe hilo uliochezwa Uwanja wa Azam Complex ulipo Chamazi, Dar es Salaam.

JKU ilikuwa inahitaji bao moja tu ili kuweza kutinga hatua hiyo, lakini ilishindikana kwani katika mechi ya kwanza ilipigwa mabao 4-1 kwenye uwanja huo huo, hivyo kuondolewa kwa jumla ya mabao 4-3.

"Wapinzani wetu wamepambana sana, walikuwa wanakaba na wanakimbia kila mahali ambapo mpira unaanguka, kusema kweli wamejituma mno tofauti na mechi ya kwanza, nawapongeza kwa hilo na katika mechi hii tumepata nafasi nne za kufunga, lakini kipa wao alikuwa mahiri akaokoa mipira iliyokuwa inakwenda wavuni," alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga na Azam FC.

Hata hivyo, Pluijm alishangazwa na jinsi mabeki wake walivyoruhusu mabao rahisi, huku akisema viungo wake walicheza mbali na walipo washambuliaji.

"Baadhi ya wachezaji wangu hawakucheza vizuri, kama huchezi ulivyoelekezwa na mechi inakuwa ngumu sana, viungo wangu walikuwa mbali kuwasapoti washambuliaji, kama hujafunga bao ni ngumu kushinda, lakini mimi kama mwalimu naona tuyaache hayo, kikubwa ni kwamba tumevuka kwenye hatua inayofuata, tutarekebisha kwenye viwanja vya mazoezini," alisema Pluijm.

Naye Kocha Mkuu wa JKU, Salim Ally, alisema pamoja na kutolewa, lakini ameridhika na jinsi vijana wake walivyocheza na wametoka kutokana na woga wa mechi ya kwanza, hivyo wamejifunza na mwakani watarudi wakiwa imara.

"Niwapongeze vijana wangu wamecheza vizuri wamefuata maelekezo, nilisema tunakuja kwenye mechi ya pili haitokuwa kama ya kwanza, niendelee kusema kuwa hofu ya vijana wangu katika mechi ya kwanza ndiyo iliyotufanya tusifuzu, kwenye mechi hii vijana wamefuata maelekezo vizuri, wamecheza vema na tumekosa nafasi nyingi za kufunga lakini huu ni mpira, ila kuna jambo ambalo tumejifunza kama mwakani tutashiriki kwenye Ligi ya Mabingwa au Kombe la Shirikisho tutakuwa wazuri kushinda," alisema.

Kwa matokeo hayo, Singida Fountaine Gate sasa itakutana na Future ya Misri, ambapo itaanzia nyumbani Septemba 15, kabla ya kwenda kumalizia ugenini jijini Cairo, Septemba 29, mwaka huu.

## Max atamba Yanga kufika mbali Afrika

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Yanga, Max Nzengeli Mpia, amesema kwa kikosi alichokikuta Yanga, ana uhakika watafika mbali kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku mwenyewe akijiandaa kuipa mafanikio klabu hiyo ili kurudia kilichofanywa msimu uliopita.

Akizungumza jiji Dar es Salaam, Max jana, raia huyo wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo pia amefichua siri ya kupenda kuchomekea jezi, akisema babu yake ambaye alikuwa mtanashati sana alipenda kuchomekea kila anapoonekana.

"Yanga tuna kikosi kizuri na kocha wetu amekuwa akikibadilisha kwa ajili ya kuwafanya wachezaji wote wacheze ili wawe kwenye ubora unaofanana, tuna timu ambayo nina uhakika itafanya vizuri huko mbele ya safari, sisi wachezaji wapya tuna deni ambalo ni kujitahidi na kuhakikisha tunapambana kwa sababu kama msimu uliopita timu ilifika fainali ya Kombe la Shirikisho, basi msimu huu sisi tunatakiwa tufanye vema kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, tufike mbali ili turudie kile ambacho wenzetu walikifanya huko nyuma," alisema mchezaji huyo ambaye pia kuna wakati uwanjani hucheza kama kiungo mshambuliaji.

## Makocha waletwa kufundisha Kabaddi

**Na Shufaa Lyimo**

VIJANA wametakiwa kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa ya kujifunza mchezo wa Kabaddi kwa lengo la kuuendeleza hapa nchini.

Akizungumza na gazeti hili juzi,wakati wa mapokezi ya makocha Nidhiyanandham Soundarajan na Simrat Satish Gaikwad kutoka nchini India, Mwenyekiti wa Chama cha Kabaddi Tanzania (TKSA), Abdala Nyoni, alisema ujio wa makocha hao utasaidia wachezaji kupata ujuzi zaidi.

Alisema makocha hao wamekuja kipindi muafaka na kuomba wadau mbalimbali nchini kujitokeza wa wingi kuwaunga mkono kwa kushiriki mchezo huo.

"Leo (juzi), tumewapokea makocha ambao wamekuja kwa lengo la kufundisha mchezo wa kabaddi, ni wakati wa vijana kutumia fursa hii kujifunza na kuufahamu kiundani," alisema Nyoni.

Nyoni alisema makocha hao wameletwa kwa ufadhili wa Serikali ya India kupitia Sports Authority of India (SAI) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Baraza la Michezo la Taifa, BMT.

"Nipende kuishukuru Serikali ya India na Tanzania kutusaidia kuleta makocha hawa kwani mategemeo yetu ni kupata maendeleo," aliongeza Mwenyekiti huyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NUNES AKARIBIA CITY

KLABU ya Manchester City inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Wolves na Ureno, Matheus Nunes, 25, baada ya kuwasilisha ofa iliyoboreshwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Express)***

### FELIX KUMRITHI SALAH

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix,23, ametambuliwa na Liverpool kama mbadala wa Mohamed Salah wa Misri,31, iwapo mchezaji huyo atahamia Saudi Arabia. ***(A Bola)***

### ALONSO AFANYA UAMUZI

MCHEZAJI anayelengwa na Manchester United, Marcus Alonso, 32, amefanya uamuzi wake juu ya uhamisho unaowezekana kwenda Old Trafford kutoka Barcelona, huku 'Mashetani Wekundu' hao wakimuona Mhispania huyo, kama mbadala wa Luke Shaw ambaye ni majeruhi. ***(Express)***

### REGUILON AWINDWA EPL

BEKI wa Tottenham Hotspur, Sergio Reguilon, 26, ni jina lingine kwenye orodha hiyo, lakini Fulham wako mbele ya Manchester United katika harakati za kumsaka Mhispania huyo. ***(Telegraph)***

### BETO MBIONI EVERTON

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Beto, 25, yuko mbioni kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 24 kutoka Udinese ya Serie A kwenda Everton, huku Toffees wakitamani kufanya biashara zaidi kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho Ijumaa. ***(iNews)***

### ADARABIOYO AWANIWA

AS Monaco imerejea kwenye mazungumzo ya kumsajili beki wa England, Tosin Adarabioyo, 25, kutoka Fulham na mazungumzo yanaendelea. ***(Fabrizio Romano)***

### VERRATTI KWENDA SAUDIA

MARCO Verratti, 30, yuko mbioni kuhama kutoka Paris St-Germain hadi Al-Arabi, baada ya klabu hiyo ya Saudi Arabia kukubaliana ada na timu hiyo ya Ufaransa kwa ajili ya kiungo huyo. ***(Sky Sport Italia)***

### ELVEDI KUNG'OLEWA

KLABU ya Everton ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili beki wa Borussia Dortmund na Uswisi, Nico Elvedi, 26. ***(Gianluca di Marzio)***

### LUKAKU HUYOOO ROMA

AS Roma imeibuka kuwa vinara wanaowania kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku, 30. ***(Fabrizio Romano)***


### SPURS NA JOHNSON

KLABU ya Tottenham Hotspur wanatazamia kufanya uhamisho wa pauni milioni 50 kumnunua mshambuliaji wa Nottingham Forest na Wales, Brennan Johnson, 22. ***(Evening Standard)***

### SA AVUTIA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest inavutiwa na mlinda mlango wa Wolves, Jose Sa, 30, huku mchezaji anayelengwa kwa muda mrefu Dean Henderson akikaribia kuhamia Crystal Palace. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GREENWOOD NJIA PANDA MAN UTD

**MANCHESTER,** England

MASON Greenwood amebaki njiapanda juu ya hatima ya soka lake baada ya Manchester United kuchukua uamuzi wa kumpiga chini na hakuna timu inayoonesha wazi kuhitaji huduma yake.

**Na sasa matumaini ya mshambuliaji huyo yamebaki kwenye klabu moja huko Albania, mahali ambako anaweza kwenda kucheza baada ya kutokuwapo na timu za kutoka Ligi Kuu tano bora za Ulaya kumhitaji.**

Greenwood mwenye umri wa miaka 21 na familia yake alikuwa na matarajio makubwa ya kurudi kuichezea Man United baada ya mabosi kuonesha wangempa nafasi nyingine ya kuonyesha ubora.

Lakini, baada ya kelele za raia wengi kupinga uamuzi wa Man United kumrudisha kutokana na kile alichofanya na kuwafanya mabosi wa miamba hiyo ya Old Trafford kutangaza kuachana naye.

●●● Julai mwaka huu, alipata mtoto na mwanamke aliyedaiwa kutaka kumbaka lakini...

Matumaini yake ya kuanza upya maisha kwenye soka yalikumbwa na pigo kubwa baada ya taarifa kutoka Italia, hasa Klabu ya AS Roma inayonolewa na Jose Mourinho iliyokuwa ikiripotiwa kuhitaji saini yake kusitisha mpango huo, huku Klabu za Saudi Pro League zikifunga milango ya kumpokea.

Greenwood alikuwa akikabiliwa na mashtaka ya jaribio la kubaka na unyanyasaji kijinsia yaliyomfanya awe nje ya uwanja muda mrefu kabla ya kufutwa.

Tangu kutokea kwa tukio hilo kumekuwa na kampeni za kutocheza tena kwenye soka la England, lakini jambo hilo limekuwa likimwandama hadi nchi nyingine na sasa matumaini yake yamebaki huko Albania, ambako kuna klabu moja inaweza kumchukua.

Julai mwaka huu, Greenwood alipata mtoto na mwanamke aliyedaiwa kutaka kumbaka.

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Man United, Richard Arnold, alisema kwenye uchunguzi maalumu uliofanywa na klabu kwa miezi mitano uligundua hakufanya kosa lolote, lakini mwenyewe ametaka kuondoka ili kwenda kuendelea na soka lake.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,148,6
MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
JKT TANZANIA
1 | 1.20
X | 5.40
2 | 11.95
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WEST HAM KUBEBA MZIGO WA MAGUIRE




**LONDON,** England

KLABU ya West Ham imerudi tena kwenye mazungumzo na Manchester United ili kuipata huduma ya beki wa kati wa 'Mashetani Wekundu' hao, Harry Maguire, kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili juma hili.

Katika mazungumzo hayo mapya, West Ham imetoa ofa ya kutaka kuisaidia Man United kulipa kiasi kidogo cha pesa kwenye kile ambacho wanatakiwa kumlipa Maguire ili aondoke.

Maguire ambaye amebakisha miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa, amedai kutaka kulipwa zaidi ya pauni milioni saba ili aondoke.

West Ham ilishafikia makubaliano ya kulipa pauni milioni 30 na kumsajili Maguire kwa mkataba wa miaka minne kisha kumlipa mshahara wa pauni 120,000 kwa wiki ikiwa ni pungufu ya pauni 70,000.

Maguire anataka fedha zaidi ama aendelee kusalia Man United ambako anaamini ndani ya miaka miwili iliyobaki atakunja pesa nyingi zaidi ya hiyo ambayo Man United ilitaka kumlipa ili aondoke.




## *Klopp aishangaa kadi ya van Dij*

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp alieleza kuwa ni "ajabu" kuona Virgil van Dijk akioneshwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya mshambuliaji wa Newcastle United, Alexander Isak kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumapili.

Van Dijk alitolewa kwa kadi nyekundu katika mechi hiyo iliyofanyika pale St James' Park, na kuiacha timu yake ikiwa na wachezaji 10 na mlima wa kupanda baada ya kuwa nyuma kwa bao moja.

Ingawa aliondoa mpira, Mholanzi huyo aliadhibiwa kwa kumzuia mpinzani wake, Isak nafasi ya wazi ya kufunga.

"Hakukuwa na muingiliano wowote kutoka kwa Virgil van Dijk. Alikwenda kutafuta mpira tu," alisema Klopp akiiambia Sky Sports baada ya mchezo huo.

Kocha huyo alikosoa katika hatua yake iliyofuata, kwani kupewa kadi nyek du ina maana kwamba Dijk atafungiwa tu mchezo mmoja badala mechi tatu. Lakini b alishangazwa ni kwa kadi nyekundu alionesh nahodha wake huyo.

"Virgil anashukuru s kwamba timu iliend kushinda. Yote ni n Wachezaji walikuja, J Quansah alikuja. Joe Go alikuja mapema na kuch mchezo mzuri, nina fu sana kwake".

S43,241/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/09/2023 | 19:30 | Brighton & Hove Albion vs Newcastle United | 2.50 | 3.55 | 2.50 |
| 02. 02/09/2023 | 19:45 | Go Ahead Eagles vs SC Heerenveen | 2.60 | 3.60 | 2.39 |
| 03. 02/09/2023 | 20:00 | Portimonense SC vs Estrela Amadora | 2.60 | 3.15 | 2.65 |
| 04. 02/09/2023 | 14:00 | Glasgow Rangers vs Celtic Glasgow | 2.36 | 3.45 | 2.75 |
| 05. 02/09/2023 | 14:30 | KAA Gent vs Club Brugge | 2.32 | 3.55 | 2.70 |
| 06. 02/09/2023 | 15:00 | FC Andorra vs Tenerife CD | 2.19 | 3.00 | 3.45 |
| 07. 03/09/2023 | 16:00 | Kalmar FF vs Mjallby AIF | 2.25 | 3.00 | 2.90 |
| 08. 03/09/2023 | 17:00 | Union Saint-Gilloise vs Royal Antwerp FC | 2.31 | 3.35 | 2.85 |
| 09. 03/09/2023 | 17:15 | RCD Mallorca vs Athletic Bilbao | 3.00 | 3.00 | 2.40 |
| 10. 03/09/2023 | 17:30 | GD Chaves vs Moreirense FC | 2.29 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 03/09/2023 | 17:30 | Estoril Praia vs Boavista Porto | 2.38 | 3.20 | 2.90 |
| 12. 03/09/2023 | 17:30 | FC Basel 1893 vs FC Zurich | 2.55 | 3.35 | 2.33 |
| 13. 03/09/2023 | 18:00 | Stroemsgodset IF vs Stabaek IF | 2.15 | 3.35 | 2.80 |
| 14. 03/09/2023 | 18:30 | IFK Norrkoping FK vs Djurgardens IF | 2.65 | 3.30 | 2.29 |
| 15. 03/09/2023 | 18:30 | Union Berlin vs RB Leipzig | 3.10 | 3.25 | 2.24 |
| 16. 03/09/2023 | 19:30 | KRC Genk vs RSC Anderlecht | 1.95 | 3.65 | 3.40 |
| 17. 03/09/2023 | 20:15 | Royal Charleroi SC vs St. Truidense VV | 2.17 | 3.35 | 3.10 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 29/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 3306 | Western Sydney vs Adelaide United | 2.21 | 3.52 | 2.75 |
| 13:00 | 3644 | Chungnam Asan vs Gyeongnam | 2.39 | 3.23 | 2.62 |
| 13:30 | 1522 | Busan I Park vs Sangju Sangmu | 2.83 | 3.34 | 2.19 |
| 13:30 | 1918 | Ansan Greeners vs Bucheon | 3.14 | 3.29 | 2.05 |
| 15:00 | 1260 | Rubin Kazan vs Ural Yekaterinburg | 2.34 | 3.10 | 2.85 |
| 16:30 | 3981 | Surkhon Termez vs Nasaf Qarshi | 4.10 | 3.05 | 1.83 |
| 17:15 | 3621 | Fakel vs Gazovik Orenburg | 2.24 | 3.36 | 2.80 |
| 17:30 | 3207 | Qizilqum vs Pakhtakor | 6.20 | 3.70 | 1.45 |
| 18:00 | 3078 | AL Akhdood vs Al Taawon | 3.51 | 3.51 | 2.00 |
| 19:00 | 1817 | Young Africans vs JKT Tanzania | 1.20 | 5.40 | 11.95 |
| 19:30 | 3236 | Spartak Moscow vs Dinamo Moscow | 1.99 | 3.71 | 3.05 |
| 19:30 | 5215 | Nizhny Novgorod vs FC Krasnodar | 3.05 | 3.20 | 2.18 |
| 20:00 | 4852 | Helsingborg vs Landskrona Bois | 2.18 | 3.41 | 3.15 |
| 21:00 | 2037 | Al Nasr Riyadh vs Al Shabab Riyadh | 1.28 | 5.45 | 9.64 |
| 21:00 | 3342 | Al Khaleej Club vs AL Hazm | 2.16 | 3.40 | 3.19 |
| 21:00 | 3862 | MK Dons vs Chelsea U21 | 2.18 | 3.61 | 2.74 |
| 21:00 | 3886 | Al Ahli Jeddah vs AL Tai | 1.29 | 5.44 | 9.20 |
| 21:30 | 1646 | AC Reggiana vs Palermo | 3.13 | 3.08 | 2.24 |
| 21:30 | 2294 | Swansea vs Bournemouth | 3.03 | 3.38 | 2.18 |
| 21:30 | 2652 | Grimsby vs Manchester City U21 | 2.37 | 3.56 | 2.51 |
| 21:30 | 2723 | Cosenza vs Modena | 2.44 | 3.13 | 2.77 |
| 21:30 | 4795 | Pisa vs Parma | 2.40 | 3.02 | 2.92 |
| 21:30 | 5630 | Ascoli vs Feralpisalo | 1.92 | 3.23 | 3.85 |
| 21:45 | 1201 | Tranmere vs Leicester | 4.99 | 3.94 | 1.59 |
| 21:45 | 1202 | Luton Town vs Gillingham | 1.29 | 5.18 | 8.77 |
| 21:45 | 1249 | Penybont vs Cardiff Met Uni. | 1.84 | 3.34 | 3.74 |
| 21:45 | 1274 | Birmingham vs Cardiff | 2.12 | 3.19 | 3.34 |
| 21:45 | 1287 | Bristol City vs Norwich City | 2.48 | 3.39 | 2.59 |
| 21:45 | 2325 | Wycombe vs Sutton United | 1.70 | 3.73 | 4.37 |
| 21:45 | 2579 | Wrexham vs Bradford City | 1.91 | 3.58 | 3.53 |
| 21:45 | 2797 | Gap Connahs Quay vs Newtown AFC | 1.60 | 3.83 | 4.44 |
| 21:45 | 3094 | Bolton vs Middlesbrough | 2.68 | 3.38 | 2.40 |
| 21:45 | 3376 | Wolverhampton vs Blackpool | 1.35 | 4.76 | 7.53 |
| 21:45 | 3584 | Newport vs Brentford | 6.19 | 4.59 | 1.42 |
| 21:45 | 3647 | Port Vale vs Crewe | 1.73 | 3.73 | 4.18 |
| 21:45 | 3683 | Caernarfon Town vs Bala Town | 3.47 | 3.62 | 1.83 |
| 21:45 | 3903 | Plymouth vs Crystal Palace | 4.18 | 3.73 | 1.73 |
| 21:45 | 3965 | Colwyn Bay vs The New Saints | 15.19 | 7.70 | 1.09 |
| 21:45 | 4209 | Sheffield Wed vs Mansfield | 1.76 | 3.68 | 4.08 |
| 21:45 | 4547 | Portsmouth vs Peterborough | 2.07 | 3.43 | 3.23 |
| 21:45 | 4638 | Barry Town FC vs Haverfordwest | 2.39 | 3.32 | 2.57 |
| 21:45 | 4962 | Fulham vs Tottenham | 3.49 | 3.59 | 1.92 |
| 21:45 | 5810 | Stoke City vs Rotherham | 1.56 | 3.99 | 5.19 |
| 21:45 | 5975 | Exeter vs Stevenage | 2.03 | 3.38 | 3.38 |
| 22:00 | 2088 | Panathinaikos vs Sporting Braga | 2.37 | 3.32 | 2.73 |
| 22:00 | 2344 | Reading vs Ipswich | 3.88 | 3.59 | 1.82 |
| 22:00 | 2844 | Galatasaray vs Molde | 1.66 | 3.68 | 4.62 |
| 22:00 | 3426 | Salford City vs Leeds | 4.50 | 3.80 | 1.67 |
| 22:00 | 4259 | BSC Young Boys vs Maccabi Haifa | 1.77 | 3.66 | 3.96 |
| 23:30 | 1235 | Cucuta Deportivo vs Club Cortulua | 1.81 | 3.32 | 4.08 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# JKT QUEENS WAIKARIBIA REKODI SIMBA QUEENS MICHUANO CAF

**Na Abdallah Mataka**

JKT Queens inaelekea kufikia rekodi ya Simba Queens ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), ambao utawapa tiketi ya kwenda kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika kwa wanawake baadaye mwaka huu.

Hiyo ni baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Buja Queens ya Burundi katika mchezo wa nusu fainali uliopigwa Uwanja wa FTC Njeru nchini Uganda

Kwa ushindi huo JKT Queens itashuka dimbani kesho kucheza fainali dhidi ya CBE ya Ethiopia ambayo iliifunga Vihiga Queens ya Kenya kwa mabao 2-1.

**Katika mchezo huo wa nusu fainali JKT Queens walikwenda mapumziko wakiwa nyuma kwa bao 1-0 lililofungwa na Teopistar Situma dakika ya 11.**

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi huku JKT wakionekana kubadilika kwani waliliandama lango la Buja Queens na dakika ya 61 Donisia Minja alifungua kitabu cha mabao akimalizia mpira uliopanguliwa na kipa wa Buja ulitokana na shuti la Stumai Abdallah.

Katika kuonesha kuwa JKT Queens wanahitaji kufuzu fainali, dakika ya 77, kiungo wake Stumai Abdallah, alifunga bao la pili akimalizia mpira wa krosi iliyopigwa na Amina Bilal na kuibua shangwe kwa mashabiki na benchi la ufundi.

Kama mbavyo mashabiki wa soka wanasema 'haiwezi kuisha hadi iishe' kabisa ndivyo ilivyokuwa kwani JKT Queens ambao walikuwa na uchu wa mabao zaidi, mshambuliaji kinda Winifrida Gerald alifunga bao la tatu dakika za nyongeza akimalizia mpira wa adhabu uliopigwa na Anastazia Katunzi baada ya Stumai kufanyiwa madhambi.

JKT Queens katika hatua ya makundi waliifunga AS Kigali ya Rwanda mabao 2-1 kabla ya kuibamiza New Generation ya Zanzibar bao 1-0 kisha kuikandamiza Vihiga Queens ya Kenya bao 1-0.

Msimu uliopita, Simba Queens ndiyo iliyouwakilisha Ukanda wa CECAFA katika michuano hiyo nchini Morocco, baada ya kutwaa ubingwa wa ukanda huu.



Mchezaji wa Timu ya Soka ya Winners Academy ya Msasani Dar es Salaam, May Abasi (wa pili kulia), akimkabilli mchezo wa Timu ya Bulls, Analise Hewitt (kulia), kwenye mchezo wa kirafika uliopigwa Mikocheni, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Peter Banda aagwa

INATOKA UKURASA 24

kupanda kileleni ni rahisi, lakini kukaa kileleni ndio ngumu zaidi, jambo la kufanya ni kuendelea kuwa na nguvu na ukifanyia kazi utafika.

"Nahitaji kuonesha kiwango kizuri na bora ili kusaidia timu yangu kuweza kufikia malengo ambayo tumejiwekea, ligi imekuwa ngumu kutokana na ushindani uliokuwapo hivyo nahitaji kuwa bora zaidi kuweza kwenda sawa na hali ilivyo," alisema Che Malone.

Katika hatua nyingine, uongozi wa klabu hiyo umeshukuru winga wake, Banda (23), huku ukimtakia mafanikio mema huko aendapo baada ya kutangaza kuachana naye.

"Katika kipindi cha miaka miwili tulichokuwa na Banda, amekuwa mchezaji muhimu ambaye alikuwa akiongeza kasi katika safu ya ushambuliaji. Simba inamshukuru na kumtakia heri Banda katika maisha yake mapya nje ya Simba," ilieleza taarifa ya klabu hiyo jana.

## *Yanga yataka mvua ya mabao kuishusha Simba*

INATOKA UKURASA 24

mwaka huu itakuwa ugenini dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan kucheza mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kutinga hatua hiyo kwa kuifurumusha ASAS FC ya Djibouti kwa jumla ya mabao 7-1, baada ya mechi ya awali kushinda 2-0 na ile ya marudiano kuibugiza 5-1.

Watani wao wa jadi, Simba, wenyewe pia watakuwa nyumbani kucheza dhidi ya Coastal Union, lakini mchezo huo haujapangiwa tarehe kutokana nao kuwa na jukumu muhimu la kimataifa kwenye Ligi ya Mabingwa, ambapo itaanzia ugenini.

# Michezo

Jumanne Agosti 29, 2023

Nipashe




Greenwood njiapanda UKURASA 21

# Yanga yataka mvua ya mabao leo kuishusha Simba kileleni

## ●●● Gamondi aeleza mkakati huku akimtaja nyota wake atakayeikosa JKT Tanzania...

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea leo kwa Yanga kucheza dhidi ya JKT Tanzania mechi yao ya raundi ya pili kabla ya kuelekea mapumziko kupisha Kalenda ya Fifa kwa ajili ya mechi za kimataifa.

**Yanga ambayo ipo nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama tatu na mabao matano huku ikiwa haijaruhusu bao hata moja, imepania kupata ushindi wa kishindo ili kuishusha Simba kileleni, ambayo ina alama sita, mabao sita ya kufunga na mawili ya kufungwa.**

Kikosi cha Yanga kitawakaribisha JKT Tanzania katika Uwanja wa Azam Complex ulipo Chamazi, Dar es Salaam huku Yanga, ambao nao wametoka kushinda mchezo wao wa awali ugenini kwa bao 1-0 dhidi ya Namungo FC.

Lakini Yanga wanashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya KMC FC, huku mashabiki wa timu hiyo ya wananchi wakitarajia kuona idadi ya mabao mengi tena.

Kuelekea mchezo wa leo, Kocha wa Yanga, Miguel Ángel Gamondi, amesema wako vizuri na walianza maandalizi juzi, ingawa kuna baadhi ya wachezaji watawakosa hilo haliwapi hofu.

"Tunawaheshimu wapinzani wetu, tukipata nafasi tutaitumia vizuri kupata idadi kubwa ya mabao kama mechi ya kwanza au laa, falsafa yangu ni kucheza mpira mzuri na kupata mabao.

"Kuhusu suala la Mahlatse Makudubela (Skudu), hatakuwa sehemu ya kikosi cha mechi ya kesho (leo) kwa sababu hakuwa katika proglamu ya mazoezi, anatakiwa kuanza mazoezi ya gym kwa muda wa wiki ili kujiweka sawa na fiti kwa mchezo ujao," alisema Gamondi.

Kocha Msaidizi wa JKT Tanzania, George Mketo, alisema wamejiandaa vizuri na wanaenda kucheza mchezo mgumu dhidi ya Yanga, ila watahakikisha wanakabiliana vema na wapinzani wao hao.

Alisema wanaenda kucheza na Yanga wakiwa na matokeo mazuri katika mechi yao iliyopita na hawaogopi wala kutishwa na matokeo ya mechi iliyopita ya wapinzani wao.

"Tumejiandaa vizuri, tumekuja kushindana na malengo yetu ni kufanya vizuri, tutacheza kwa umakini na kuwaheshimu Yanga kulingana na ubora wa wapinzani wetu kwa kila nafasi," alisema Mketo.

Baada ya mechi hiyo timu hizo zitaelekea mapumziko kupisha Kalenda ya Fifa inayotarajiwa kuanza Septemba 4-12, huku Ligi Kuu Bara ikitarajiwa kurejea tena Septemba 15, mwaka huu kwa JKT Tanzania kuwa ugenini tena dhidi ya KMC FC.

Kwa Yanga mchezo ujao utakuwa nyumbani tena dhidi ya Namungo FC, lakini haujapangiwa tarehe, kwani Septemba 15-17,

INAENDELEA UKURASA 23



Maxi Mpia Nzengeli. **Habari ukurasa 20.**

# Banda aagwa, Robertinho atoa kazi za nyumbani

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, akiwapa programu maalum wachezaji wa timu hiyo, kipindi chote cha mapumziko huku akiwataka kurudisha ripoti kwake kwa kile walichokifanya kulingana na mazoezi ambayo wamefanya, uongozi wa klabu hiyo umetangaza kuachana rasmi na winga Mmalawi Peter Banda.

Robertinho ametoa kauli hiyo kwa kusema watakuwa na mapumziko ya muda mrefu, hivyo wachezaji hawatakiwi kupumzika na kila mmoja amempa programu maalum ya mazoezi kuhakikisha mwisho wa siku anawasilisha ripoti ya maendeleo ya kile alichokifanya.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema wachezaji wake hawawezi kukaa kambini kwa muda mrefu hasa muda ambao ligi imesimama, hivyo ameamua kuwapa kazi ya kufanya kwa kuwa anataka wawe bora wakati wote kutokana na mashindano yaliopo mbele yao.

Alisema wako kwenye mapumziko mafupi kupisha Kalenda ya Fifa, lakini wachezaji wake hawana muda wa kupumzika na wataendelea na majukumu yao ya mazoezi maalum na kila mmoja kuwasilisha kile anachokifanya kulingana na programu aliyompa.

"Nahitaji wachezaji wangu wote watakaporejea kambini wanakuwa fiti na uwiano mzuri wa mazoezi, kwa sababu kuna baadhi ya nyota wengine watakuwa katika majukumu ya mataifa yao (timu zao za taifa).

"Hakuna muda wa kupoteza kwa sababu tuna kibarua cha mechi yetu ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos, tushinde huu mchezo ili kusonga hatua ya makundi," alisema Robertinho.

Naye beki wa timu hiyo, Che Fondoh Malone, alisema kulingana na ushindani uliopo hana muda wa kumpumzika na atautumia kufanya programu zaidi ya kile alichokipewa na kocha wao Robertinho.

"Hakuna likizo, hakuna muda wa kupumzika ni kazi tu ili

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >